RIPOTI YA KAMATI YA FEDHA, BIASHARA NA KILIMO
YA BARAZA LAWAWAKILISHI ZANZIBAR
KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

SEHEMU YA KWANZA

UTANGULIZI

Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ni miongoni mwa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi iliyoundwa kwa mujibu wa Jadweli la Kwanza la Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2016. Katika kutekeleza majukumu yake Kamati hii imetakiwa kufanya shughuli zifuatazo:

(a) Kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa kwenye ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia.

(b) Kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Wizara husika kwa kadiri Spika atakavyoelekeza kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa Barazani wakati wa usomaji Bajeti na Hotuba nyengine za Waziri alizotoa katika Baraza.

(c) Kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Kitaifa na Miradi ya Wananchi ya Wizara husika.

(d) Kuchunguza na kufatilia mapato na matumizi ya kila mwaka ya Serikali na kama matumizi yaliyofanywa yalizingatia thamani halisi ya fedha.

(e) Kuchambuwa mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya Wizara husika ya mapato na matumizi ya kila mwaka.

(f) Kushughulikia Miswada ya Sheria itakayokabidhiwa kwake na Spika.

(g) Kuchambuwa ahadi zote za Wizara zilizo chini ya Kamati kama zitakavyokuwa zikitolewa katika Baraza na kufatilia utekelezaji wa ahadi hizo.

(h) Kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa kwake na Spika.

Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo imepangiwa kusimamia Wizara zifuatazo:

- Wizara ya Fedha na Mipango
- Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi.
- Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

MUUNDO WA KAMATI

Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ina Wajumbe saba na Makatibu wawili, naomba kwa ruhusa yako niwatambue kwa majina Wajumbe na Makatibu hao kama hivi ifuatavyo:

1. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Mwenyekiti
2. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Ali Salum Haji	-	Mjumbe
4. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Mjumbe
5. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Mjumbe
6. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	-	Mjumbe
7. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Mjumbe
8. Ndg. Salum Khamis Rashid	-	Katibu
9. Ndg. Asma Ali Kassim	-	Katibu

UTARATIBU WA KAZI ZA KAMATI

Kwa mujibu wa Kanuni ya 108 (8), Kamati ilifanya kazi zake kwa utaratibu wa kupokea taarifa za utekelezaji wa malengo ya Wizara, kupokea taarifa za utekelezaji wa Maagizo ya Kamati, Kukutana na wadau mbali mbali wa sekta zinazosimamiwa na Kamati na kukagua baadhi ya maeneo ili kuona hatua za utekelezaji zilizofikiwa.

Kwa mwaka huu wa fedha 2016/2017, hadi Kamati inawasilisha ripoti yake mbele ya Baraza hili tukufu ilifanya kazi zake katika mizunguko mitatu kwa muda wa wiki sita, kati ya Unguja na Pemba.

- Mzunguko wa kwanza kuanziaTarehe 29/08/2016 hadi 09/09/2016 - Unguja.
- Mzunguko wa pili kuanzia Tarehe 31/10/2016 hadi tarehe 04/11/2016 – Pemba na Tarehe 07/11/2016 hadi Tarehe 11/11/2016 - Unguja.
- Mzunguko wa tatu kuanzia Tarehe 16/01/2017 – hadi tarehe 20/01/2017 - Unguja na Tarehe 23/01/2017 hadi Tarehe 27/01/2017 – Pemba.

SEHEMU YA PILI

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

Wizara ya Fedha na Mipango imeundwa na Idara kumi (10), Tume ya Mipango yenye Idara nne (04), Taasisi Tisa (09) zinazojitegemea na Taasisi nne (04) za Muungano zinazofanya kazi hapa Zanzibar. Idara na Taasisi hizo ni kama ifuatavyo:

IDARA ZA WAZARA YA FEDHA NA MIPANGO

I. Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali
II. Idara ya Bajeti
III. Idara ya Fedha za Nje
IV. Idara ya Uhakikimali
V. Idara ya Mitaji ya Umma

VI. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti
VII. Idara ya Hesabu za Ndani
VIII. Idara ya Utawala na Uwendeshaji
IX. Idara ya Fedha za Kodi
X. Ofisi Kuu Pemba

TUME YA MIPANGO

I. Idara ya Uratibu wa Mipango ya Kitaifa, maendeleo ya kisekta na kupunguza umasikini
II. Idara ya Maendeleo ya Watendakazi
III. Idara ya Ukuzaji Uchumi
IV. Idara ya Ufuatiliaji na Tathmini

TAASISI ZINAZOJITEGEMEA

I. Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB)
II. Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ)
III. Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi (ZIPA)
IV. Mfuko wa Barabara (ZFR)
V. Shirika la Bima la Zanzibar (ZIC)
VI. Bodi ya Rufaa za Kodi (Tax Appeal Board)
VII. Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF)
VIII. Mahkama ya Rufaa za Kodi
IX. Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali

TAASISI ZA MUUNGANO

I. Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)
II. Mamlaka ya Bima Tanzania (TIRA)
III. Benki Kuu ya Tanzania (BOT)
IV. Tume ya Pamoja ya Fedha – Tawi la Zanzibar

UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA KAMATI YALIYOTOKANA NA RIPOTI YA KAMATI YA MWAKA 2014/2015

Kamati katika kutekeleza kazi zake iliitaka Wizara kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa Maagizo ya Kamati yaliyotokana na Ripoti ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Kwa ujumla Kamati iliridhishwa kwa hatua zilizofanywa katika kutekeleza kwa baadhi ya maagizo na maoni ya Kamati. Isipokuwa Kamati yetu inaendelea kusisitiza katika maagizo yafuatayo;

Kamati iliyopita iliishauri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ishirikiane na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Makao Makuu ili kasoro iliyopo ya kumfanya Naibu Kamishna wa TRA Zanzibar kuwa katika ngazi ya nne katika ngazi za uongozi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ambaye anawajibika kwa Kamishna wa Forodha iweze kurekebishwa. Kamati ilielezwa utekelezaji wa agizo hili kuwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ipo katika hatua za mwisho za kuanza kufanya marekebisho ya muundo wa Mamlaka kwa kushirikiana na mshauri elekezi ili kuandaa mapendekezo ya kubadilisha muundo huo ili kuendana na mazingira mapya ya

kiuchumi, kijamii na kisiasa. Ni matumaini ya Serikali kuwa Muundo mpya wa Mamlaka utaweza kuondoa tatizo lililopo hivi sasa.

Kamati yetu inaendelea kusisitiza kuharakishwa marekebisho ya muundo huo wa uongozi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) uliopo hivi sasa, kwani hii imekuwa ni kero ya muda mrefu na Kamati zilizopita zimekuwa zikilizungumzia suala hili mara kwa mara. Tunaomba sana utekelezaji wa agizo hili kwa hatua iliyofikia ufanywe kwa haraka ili kuondoa kero hii ya muda mrefu. Vile vile Wizara isimamie utekelezwaji wa makubaliano ya ajira ya asilimia 29 kwa Zanzibar na asilimia 79 kwa Tanzania Bara kwa TRA.

Vile vile, Kamati iliishauri Wizara kuifanyia marekebisho Sheria ya Mfuko wa Barabara ambayo inatumika. Hivyo, Sheria hiyo irekebishwe ili kuwepo kwa ushirikishwaji wa kutosha kwa Mfuko wa Barabara hususan katika uingiaji wa mikataba pamoja na utekelezaji wa shughuli za utengenezaji wa barabara. Katika kutekeleza agizo hili, Kamati yetu ilielezwa kuwa, ni kweli Sheria iliyopo ya Mfuko wa Barabara imeonekana kuwa na mapungufu ambao unachangia kupunguza uwezo wa Mfuko katika kutekeleza majukumu yake. Kutokana na hali hiyo Bodi ya Mfuko wa barabara kwa upande wake imeshaanzisha mchakato wa kupitia Sheria iliyopo ili kuorodhesha maeneo ya upungufu ambayo yatawasilishwa mbele ya wadau wa Mfuko wa Barabara kwa kupata maoni kabla ya kupelekwa Serikalini.

Kutokana na umuhimu wa kuwepo kwa Mfuko huu wa Barabara ambao matunda yake yanaonekana, lakini kumekuwepo na baadhi ya kasoro katika Sheria iliyoanzisha Mfuko huo Sheria Namba 2 ya 2001 ambazo hata Kamati yetu imeziona. Kamati yetu inashauri kufanywa marekebisho ya Sheria hii, kutokana na kasoro zilizopo ili iendane na wakati na kwa mujibu wa mahitaji yaliyopo.

UTEKELEZAJI WA BAJETI

Kwa mwaka wa Fedha 2016/17, Wizara ya Fedha na Mipango imekadiriwa kukusanya jumla ya TZS 824.35 bilioni ikiwa ni ongezeko la TZS 7.09 bilioni ikilinganishwa na makadirio ya mwaka 2015/16 ya TZS 817.26 bilioni.

Kwa upande wa Matumizi Wizara ya Fedha na Mipango imepangiwa kutumia jumla ya TZS 157.69 bilioni kwa matumizi ya F01- Wizara ya Fedha na Mipango, F02- Mfuko Mkuu wa Serikali na F03- Tume ya Mipango.
Kwa kupitia programu mbali mbali za Wizara, Bajeti ya mwaka 2016/17 ilijikita katika kutekeleza shughuli zifuatazo:

I. Kuanza ujenzi wa ofisi mpya ya Pemba inayohusisha pia ofisi ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto pamoja na ofisi ya Rais-Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora;
II. Kusimamia upatikanaji wa mapato ya Serikali ya TZS 824.35 bilioni ili kukidhi mahitaji ya matumizi ya Serikali;
III. Kusimamia ulipaji wa madeni ya kiinua mgongo kwa wastaafu wa Serikali ili kurejesha utaratibu wa madeni hayo yasipindukie miezi mitatu;
IV. Kujenga mfumo wa ufuatiliaji na tathmini wa Mkakati wa maendeleo Zanzibar pamoja na muongozo wake;

V. Kukamilisha uandaaji wa sharia mpya ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma, na marekebisho ya Sheria ya Hifadhi ya Jamii.

Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara ilikadiriwa kukusanya jumla ya TZS 8,322.00 milioni kutoka vyanzo tofauti vya Mapato. Kwa upande wa Matumizi, Wizara ilikadiria kutumia TZS 157,691.40 milioni ili kutekeleza programu kuu zifuatazo:

I. Usimamizi wa Hazina ilikadiriwa kutumia TZS 29,558.11 milioni
II. Usimamizi wa Bajeti na Fedha za Umma ilikadiriwa kutumia TZS 22,740.00 milioni
III. Uratibu wa Rasilimali za Nje ilikadiriwa kutumia 1,515.46 milioni
IV. Usimamizi wa uwekezaji wa Mali za Umma ilikadiriwa kutumia TZS 6767.58 milioni
V. Mipango na Uendeshaji wa Sekta ya Fedha ilikadiriwa kutumia TZS 7,284.82 milioni
VI. Usimamizi wa Mfuko Mkuu wa Serikali ulikadiriwa kutumia TZS 83,529.90 milioni
VII. Mipango ya Kitaifa na Maendeleo ya Watendakazi ilikadiriwa kutumia TZS 688.71 milioni
VIII. Usimamizi wa Uchumi Mkuu ilikadiriwa kutumia TZS 3,071.53 milioni na
IX. Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Mipango ilikadiriwa kutumia TZS 376.95 milioni

UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA NUSU MWAKA (JULAI-DISEMBA 2016) KWA MWAKA WA FEDHA 2016/17

UKUSANYAJI WA MAPATO

Katika kipindi cha Julai- Desemba 2016, Wizara imekusanya jumla ya TZS 249.47 bilioni ikiwa ni sawa na asilimia 30 ya makadirio ya TZS 824.36 bilioni yaliotarajiwa kukusanywa kwa mwaka 2016/17. Mapato hayo yaliyokusanywa yanajumuisha TZS 124.44 bilioni zilizokusanywa na Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB), TZS101.29 bilioni zilizokusanya na Mamlaka ya Mapato ya Tanzania- Tawi la Zanzibar, TZS 10.50 bilioni zilipokelewa ikiwa ni PAYE kwa Wafanyakazi wa Jamuhuri wanaofanya kazi hapa Zanzibar, Mapato ya Wizara ni TZS13.24 bilioni na TZS 0.37 bilioni zilipokelewa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Uchanganuzi wa Mapato hayo unaonekana katika Jadueli nam. 1.

Mapato yaliyosimamiwa na Wizara ya Fedha na Mipango kwa kipindi cha Oktoba-Disemba 2016
Jadueli no. I

TAASISI	**MAKADIRIO YA MWAKA (bilioni)**	**UKUSANYAJI HALISI (bilioni)**	**ASILIMIA YA MAKADIRIO YA MWAKA (%)**
MAPATO YA NDANI			
BODI YA MAPATO (ZRB)	237.44	124.45	52
MAMLAKA YA MAPATO (TRA)	188.80	101.29	54
PAYE SMT	21.00	10.50	50
MAPATO YASIYOKUWA YA KODI	18.02	13.24	73

MIKOPO YA NDANI	33.00		
JUMLA NDOGO	**498.26**	**249.48**	**50**
MAPATO KUTOKA KWA WASHIRIKA WA MAENDELEO	326.10	0.37	0.1
JUMLA KUU	**824.36**	**249.85**	**30**

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

USIMANIZI WA MATUMIZI YA SRIKALI

Miongoni mwa majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango ni kuzigawanya rasilimali fedha zilizopatikana katika Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali ili kutekeleza Mipango ya Serikali. Kwa ujumla, matumizi ya Serikali katika kipindi cha Julai–Disemba 2016 yamefikia TZS 247.97 bilioni sawa na asilimia 30 ya makadirio ya kipindi hicho cha tathmini. Uchambuzi wa matumizi hayo unaonekana katika jadueli namba II.

Katika kipindi cha utekelezaji wa nusu mwaka 2016/2017, Wizara imefanikiwa kulipa viinua mgongo vyenye thamani ya TZS 4.99 milioni kwa wastaafu 234 kwa taarifa za wastaafu zilizopokelewa Wizarani katika kipindi cha Juni 2016 hadi Agosti 2016.

MATUMIZI YA SERIKALI KWA KPINDI CHA JULAI-DISEMBA 2016
Jadueli no. II

MAELEZO	**MAKADIRIO KWA MWAKA 2016/17**	**MATUMI HALISI**	**ASILIMIA (%)**
MATUMIZI YA KAWAIDA	**Tarakimu (TZS Bilioni)**		
MISHAHARA	223.7	99.43	44
MATUMIZI MENGINEYO	80.6	46.55	56
RUZUKU	59	28.50	48
MATUMIZI YA MFUKO MKUU WA SERIKALI	82.3	50.26	61
JUMLA NDOGO (A)	**445.6**	**224.74**	**50**
MATUMIZI YA MAENDELEO			
a) MCHANGO WA SERIKALI	71.1	23.24	33
b) MCHANGO WA WASHIRIKA WA MAENDELEO	324.8	0.37	0.1
JUMLA NDOGO(B)	**395.9**	**23.61**	**33**
JUMLA KUU (A+B)	**841.5**	**248.35**	**30**

MATUMIZI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

Wizara ya Fedha na Mipango imetumia jumla ya TZS 73,225.78 milioni sawa na asilimia 46 ya makadirio ya TZS 157,691.40 milioni zilizokadiriwa kutumika katika kipindi cha robo mbili ya mwaka wa fedha 2016/17.

PROGRAMU KUU YA USIMAMIZI NA UWEKEZAJI WA MALI ZA UMMA

Program hii inasimamia suala ziama la Usimamizi na Uwekezaji wa Mali za Umma na Usimamizi wa Manunuzi na Uhakiki wa Mali za Serikali ambapo jumla ya Tshs. 6,767,582 zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza Programu hii. Katika kufuatilia Programu hii, Kamati imebaini kuwa bado zipo kasoro katika suala zima la Manunuzi ya Mali za Umma kwa kutokufuatwa Sheria na taratibu za Manunuzi kwa baadhi ya Taasisi za Serikali. Nidhamu katika manunuzi ya Mali za Umma inatakiwa kusimamiwa kwa hali zote kwani takriban asilimia 70 ya Fedha za Umma zinakwenda kwenye manunuzi. Kasoro hizi zinasababishwa na kutowepo kwa watalamu wa kutosha na vile vile uwajibikaji mdogo kwa baadhi ya maafisa wanaosimamia fedha za umma.

Vile, katika usimamizi wa mali za Umma, Kamati imeona kuwa bado yapo mapungufu katika kusimamia mali za Umma, kwa mfano Kamati ilihoji katika maeneo yafuatayo:

MADENI YA MASHAMBA YA MIPIRA

Kamati yetu wakati ikiwa katika ziara zake, ilifanya ziara katika mashamba ya Mipira kisiwani Pemba, katika ziara hiyo Kamati ilikutana na viongozi pamoja na wakulima wanaoyashughulikia mashamba hayo ambao wameunda kikundi kinachojulikana kwa jina la JIWEZESHE GROUP. Kabla ya mashamba hayo kutumiwa na kikundi hiki, Serikali kupitia Wizara ya Fedha iliingia mkataba na Kampuni ya AGROTEX ambapo Kampuni ilitakiwa kulipa USD 100,000/- (Dola laki moja) kwa kila mwaka. Hatima yake, Kampuni hii ilishindwa kulipa fedha hizo kwa Serikali kwa kipindi cha miaka minne (4) na vile vile iIishindwa kulipa mishahara kwa wafanyakazi. Hadi Kamati yetu inawasilisha Ripoti mbele ya Baraza hili, Kampuni hii inadaiwa na Serikali USD 400,000/- (Dola laki nne) kama ni kodi ya mashamba hayo.

Wafanyakazi ambao walikuwa wanayashaghulikia mashamba haya, waliamua kujikusanya pamoja na kuunda kikundi hicho kwa ajili ya kuendeleza shughuli za uvunaji wa mpira. Idhini ya matumizi ya mashamba hayo yalitolewa na Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini – Pemba kupitia barua ya tarehe 10 Februari, 2016 yenye Ref: NO. MKP/K.6/3/1/VOL.VII/115.

Kamati yetu haikuridhishwa na uidhinishaji wa matumizi ya mashamba hayo uliofanywa na Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba. Kwani wakati uamuzi huu unafanywa mkataba kati ya Serikali na AGROTEX bado haujavunjwa.

Vile vile, Kamati yetu imesikitishwa sana kuona kuwa azma ya kuanzishwa kwa mashamba haya ambayo ilikuwa ni kuinua pato la Taifa na uchumi wa nchi haijafikiwa, kwani mapato mengi ya Serikali yaliyokusudiwa kuingia katika Mfuko wa Serikali kupitia mashamba haya yamepotea.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Serikali ihakikishe deni linalowadai Kampuni ya AGROTEX lifuatiliwe na liweze kulipwa haraka iwezekanavyo.

2. Serikali isitishe mara moja uvunaji wa mipira katika mashamba yote yaliyopo Zanzibar ili kuangalia namna bora ambayo itaweza kunufaisha wafanyakazi wanaoshughulikia mashamba hayo na kuona kuwa mapato ya Serikali yanayotokana na mashamba haya yanapatikana.

3. Serikali ivunje mkataba baina ya Kampuni ya AGROTEX na Wiizara ya Fedha ili mashamba haya yarudi katika mikono ya Serikali.

4. Wizara ifatilie mchakato mzima wa uvunaji wa mpira, uuzaji na usafirishaji ili kuona kuwa wanaonunua mpira na kuusafirisha nje ya nchi wanalipa kodi ipasavyo, na jee Kampuni ya AGROTEX haihusiki katika ununuzi huo.

5. Serikali ianzishe utaratibu maalumu wa ushughulikiaji wa mashamba haya, kwani baadhi ya mashamba yanaonekana kuwa yamezungukwa na msitu mkubwa jambo ambalo linahatarisha uhai wa miti hiyo, na vile vile kwa kushirikiana na Wizara ya kilimo kuangalia namna ya kupanda miti mipya ya mipira kwani miti mingi tayari imeshazeeka.

MAGHALA YA SERIKALI

Kamati yetu iliomba kupatiwa orodha ya maghala ya Serikali kwa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko na Kamati ilipatiwa orodha hiyo. Kwa mujibu wa taarifa hiyo, baada ya kuvunjwa kwa Shirika la Bizanje Serikali ilikabidhiwa jumla ya Maghala Thelathini na nne (34) na Kampuni 25. Kati ya Maghala na Kampuni hizo, kuna ambazo zipo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko pamoja na Wizara ya Mawasiliano Ujenzi na Usafirishaji. Na katika Maghala na Kampuni hizo yapo mabayo yameuzwa, yaliyokodishwa na yanayotumika kama ni Afisi za Serikali. Takribani maghala saba (7) yameuzwa na majengo nane (8) yaliyokuwa Kampuni yameuzwa.

Vile vile, Kamati yetu ilibahatika kutembelea baadhi ya maghala ya Serikali na haikuridhishwa na hali maghala hayo kwani yapo katika hali mbaya sana.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Serikali itamke wazi kupiga marufuku uuzaji wa maghala ya Serikali na majengo yaliyokuwa Kampuni za Serikali ili kunusuru majengo yaliyopo yasitoweke na yaweze kutumika katika shughuli mbali mbali.

2. Wizara ifanye mapitio ya mikataba ya ukodishwaji wa majengo ya Serikali ili kuona kiwango halisi cha malipo yanayolipwa sasa hivi yanaendana na mahala lilipo jengo na wakati tulionao.

3. Wizara ya Fedha kupitia Idara ya Uhakikimali, ifanye tathmini na mapitio kwa majengo yote yaliyokuwa maghala ya Serikli na Makampuni ili kupata idadi halisi ya majengo hayo ambayo yapo Serikalini kwa sasa.

4. Serikali itenge fedha maalumu katika bajeti yake ili kufanya ukarabati wa maghala yote ambayo ni mabovu ili yasijekuanguka na kufanywa kuwa ni magofu.

MRADI WA UJENZI WA UKUTA WA FORODHANI

Mradi huu ni moja ya miradi inayosimamiwa chini ya Mradi wa ZUSP ambao Kamati yetu ilifanya ziara katika ujenzi huo. Kamati yetu inaipongeza sana Serikali kupitia Wizara ya Fedha kwa kiasi kikubwa kukamilisha mradi huu, jambo ambalo litasaidia sana kuweka mandhari nzuri ya mji wa Zanzibar na kuwa kivutio kwa wanaotembelea katika eneo la Mji Mkongwe hasa watalii.

Mradi kwa gharama za awali ulihgarimu jumla ya Shilingi 8,000,000,000, hata hivyo kutokana na kasoro zilibainika baada ya kuanza ujenzi huo kumekuwa na ongezeko la fedha mbali ya fedha zilizokubaliwa awali. Ongezeko hili limetokea baada ya kuona kuwa barabara kubwa inayoelekea Forodhani imepata athari kubwa ya kuchimbuka mashimo kwa maji ya bahari na hivyo kulazimu pia kujengwa upya kwa barabara hiyo ili kuwanusuru watumiaji wa njia hiyo.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

Serikali iwe angalifu sana wakati wanapotafuta washauri elekezi katika Miradi ya Serikali na kuwapa hadidu rejea ambazo wataweza kuishauri Serikali ipasavyo ili kuweza kuepuka gharama za ziada ambazo zinaweza kuepukika.

MRADI WA UJENZI WA JENGO JIPYA LA WIZARA – GOMBANI, PEMBA

Mradi huu ni moja ya miradi inayosimamiwa chini ya Mradi wa Ujenzi wa Afisi za Serikali ambao Kamati yetu imefanya ziara mara mbili katika ujenzi huo. Kamati inatoa pongezi za dhati kwa jitihada za Serikali kuwa na mradi huu wa ujenzi wa Afisi za Wizara kwa upande wa Pemba, Kamati ilielezwa kuwa ujenzi huu utachukuwa Wizara tatu kwa Pemba. Ni wazi kuwa kukamilika kwa jengo hili kutapunguza changamoto kubwa iliyopo Pemba ya upungufu wa majengo ya Wizara. Kamati yetu imeridhishwa na maendeleo ya ujenzi wa jengo hili kwani Kamati inafatilia kwa ukaribu sana maendeleo ya ujenzi huu.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Wizara iwe makini wakati ujenzi unaendelea ili Serikali isijekupata gharama za ziada wakati ujenzi unaendelea (extra cost).

2. Wizara ihakikishe kuwa fedha zinapatikana kwa wakati ili ujenzi uweze kumaliza kwa wakati kwa mujibu wa makubaliano.
3. Wizara ihakikishe inafatilia hatua kwa hatua ujenzi huo ili kuhakikisha jengo hili linakuwa madhubuti baada ya kukamilika kwake.

DENI LA TAIFA

Katika robo ya pili ya mwaka wa fedha 2016/2017, hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2016, Deni la Taifa limefikia Tzs. 369.90 Bilioni ambalo ni upungufu wa Tzs. 4.8 bilioni ikilinganishwa na deni lililokuwepo tarehe 30 Novemba, 2016. Upungufu huu umetokana na kulipa deni la viinua mgongo kwa wastaafu wa mwezi wa Ogasti 2016, kufanya malipo ya wazabuni na kurejesha mkopo wa PBZ.

Deni la nje liliripotiwa kwa mwezi wa Disemba, 2016 ni Tzs. 261.7 bilioni ikiwa na upungufu wa Tzs. 1.2 bilioni uliosababishwa na mabadiliko ya sarafu za kigeni kwa kulinganishwa na Deni lililokuwepo katika mwezi wa Novemba, 2016. Mchanganuo huu unaonekana katika jadweli la hapa chini.

AINA YA DENI	DISEMBA, 2016
	TZS BILIONI
HATI FUNGANI ZA MUDA MREFU	60.30
KIINUA MGONGO	5.00
WAZABUNI WA SERIKALI	6.90
MADENI MENGINEYO	36.00
DENI LA NJE	261.70
JUMLA	**369.90**

AFISI YA MUHASIBU MKUU WA SERIKALI

Kamati inatoa pongezi kwa Mhasibu mkuu wa Serikali kwa kuhakikisha kuwa malengo ya Serikali katika kufikia utekelezaji wa bajeti ya Serikali yanafikiwa. Hata hivyo, Kamati inamtaka Muhasibu mkuu kuwasimamia ipasavyo wahasibu na washika fedha wote wa Serikali ili kuhakikisha mapato na matumizi ya fedha za umma yanatumika kwa maslahi ya umma na sio kwa maslahi binafsi na yawe yanazingatia thamani halisi ya fedha (value for money).

Vile vile, Kamati imeridhishwa na utaratibu ulioanzishwa kwa baadhi ya Tasisi za Serikali kuanza kukusanya mapato kupitia Bank moja kwa moja na kuachana na utaratibu wa kufanya malipo kwa njia ya *cash.*

Kamati inamtaka Mhasibu Mkuu wa Serikali kuhakikisha kuwa, ifikapo bajeti ya mwakani malipo yote ya Serikali kwa Taasisi zake zote yanalipwa kupitia Bank ili kuongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato na kupunguza mianya ya uvujaji wa mapato ya Serikali.

BODI YA MAPATO ZANZIBAR (ZRB)

UTEKELEZAJI WA MALENGO YA UKUSANYAJI WA MAPATO KWA BODI YA MAPATO ZANZIBAR

Kamati yetu inatoa pongezi kwa Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) kwa juhudi zao kubwa wanazozifanya ili kuhakikisha mapato ya nchi yanakusanywa kwa mujibu wa malengo yaliyokusudiwa na Serikali. Katika mwaka huu wa fedha 2016/2017 Bodi katika kipindi cha miezi sita kuanzia Julai hadi Disemba, 2016 imekadiria kukusanya mapato jumla ya TSHS. 133.24 Bilioni kutokana na vianzio mbali mbali inavyovisimamia. Makusanyo halisi yaliyokusanywa ni TSHS. 138.75 Bilioni ambazo ni sawa asilimia 104.14 ya makadirio. Ikilinganishwa baina ya makusanyo yaliyofikiwa ya TSHS. 138.75 Bilioni kwa miezi sita na makadirio ya mwaka ya TSHS. 272.64 Bilioni, inajionesha kwamba makadirio ya mwaka yametekelezwa kwa asilimia 50.89. Ikilinganishwa na kipindi kama hiki mwaka wa fedha 2015/2016 makusanyo yalikuwa Tshs. 103.91 bilioni ambapo ongezeko la makusanyo limefikia Tshs.34.84 bilioni

Pamoja na pongezi hizi, Kamati yetu inaitaka Bodi ya Mapato Zanzibar izidishe jitihada zaidi katika kuhakikisha kuwa mapato yanaongezeka kwa kasi kubwa, kwani tunaamini kuwa yapo maeneo mengi yanayotakiwa kulipa kodi bado hayajafikiwa na pia wapo baadhi ya wafanyabiashara ambao hushirikiana na watumishi wa umma wasiokuwa waadilifu kukwepa kulipa kodi za Serikali. Kamati kwa kushirikiana na Wajumbe wa Baraza la Wawawikishi itatoa mashirikiano kwa Bodi ya Mapato ya Zanzibar kuwafahamu wanaokwepa kulipa kodi.

MUHTASARI WA MAKADIRIO YA MAKUSANYO HALISI KWA MUJIBU WA VIANZIO KWA KIPINDI CHA MIEZI SITA JULAI – DISEMBA

KIANZIO	MAKADIRIO (BILIONI)	MAKUSANYO (BILIONI)	UTEKELEZAJI (%)
Kodi ya Ongezeko la Thamani	39.17	49.72	126.93
Ushuru wa Bidhaa	12.73	6.14	48.24
Ushuru wa Hoteli	7.86	9.15	116.38
Ushuru wa Mikahawa	1.97	1.77	89.82
Ushuru wa Watembeza Wageni	0.86	0.73	85.39
Ushuru wa Stempu	2.70	2.06	76.26
Ada wa huduma za Uwanja wa Ndege	13.65	15.52	113.68
Ada ya Huduma za bandarini	1.69	2.33	138.33
Mfuko wa MAendeleo ya Barabara	4.62	4.64	100.43
Ushuru wa Bidhaa za Petroli	17.36	18.67	107.59
Mapato ya Mawizara	16.09	13.24	82.28
Ada wa Usajili wa Vyombo vya Moto	0.57	0.48	84.51
Ada ya Leseni ya Njia	1.59	1.62	101.71
Ada ya Leseni ya Udereva	0.80	0.74	92.32
Ada ua Usalama wa Uwanja wa Ndege	3.16	3.50	110.85
Kodi ya Miundombinu	8.40	8.42	100.20
JUMLA	**133.24**	**138.75**	**104.14**

CHANZO: ZRB

CHANGAMOTO

Pamoja na mafanikio yanayoonekana kwa Bodi ya Mapato Zanzibar, lakini bado Bodi inakabiliwa na Changamoto zifuatazo:

(a) Ukosefu wa jengo la Afisi ya Bodi ya Mapato Zanzibar – Pemba.

(b) Kutokuwepo kwa utamaduni wa kulipa kodo kwa hiari kwani inaonekana kuwa bado kuna baadhi ya walipakodi wamejenga tabia ya kukwepa kulipa kodi.

(c) Kutokutolewa kwa risiti kwa walipakodi wanapofanya mauzo au manunuzi katika maeneo ya biashara zao.

(d) Kuwepo kwa magendo ya mafuta hapa nchini.

(e) Kuwepo kwa nyumba zinazolaza wageni bila ya kusajiliwa na Bodi (Hoteli bubu).

(f) Kutokupatikana kwa taarifa sahihi za walipakodi hasa katika maeneo ya mahoteli na mikahawa.

(g) Mapato mengi ya watalii kupotea kupitia kwa mfumo wa package tourism.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Serikali iangalie uwezekano wa kuwapatia Afisi ya kudumu ZRB kwa upande wa Pemba.

2. Elimu izidi kutolewa kwa wananchi ili wafahamu umuhimu wa kulipa kodi na kudai risiti.

3. Operesheni za mara kwa mara ziendelee kufanywa katika maeneo mbali mbali yanayokwepwa kulipa kodi kwa Unguja na Pemba.

4. Serikali iendelee kutoa boti na vifaa vya kisasa kwa Kikosi Maalumu cha Kuzuia Magendo (KMKM) ili kuimarisha zaidi ulinzi katika maeneo ya bahari yetu na kukomesha magendo ya mafuta.

5. Bodi ya Mapato ikae pamoja na Kamisheni ya Utalii ili kujadili na kuona ni namna gani wanaweza kudhibiti upatikanaji wa mapato kwa watalii wanaoingia kwa mfumo wa package tourism.

6. Uongozi wa Bodi ya Mapato uhakikishe inawasimamia watendaji wake ipasavyo katika kuhakikisha wanakuwa waadilifu katika kutekeleza majukumu yao, na Bodi isisite kuchukuwa hatua za kinidhamu au kisheria kwa mtendaji yeyote atayebainika kwenda kinyume na maadili ya kazi zake.
7. Bodi isimvumilie mlipakodi yeyote atayebainika kukwepa kulipa kodi, na ihahakikishe kuwa atayebainika kufanya hivyo anafikishwa katika vyombo vya Sheria.

8. Kuendelea kufanya ziara za kushtukiza katika maeneo mbali mbali ikiwemo mahoteli na mikahawa ili kuwabaini wanaokwepa kulipa kodi katika maeneo yote ya Unguja na Pemba.

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA – ZANZIBAR (TRA)

Kamati yetu inaendelea kuipongeza Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa juhudi za ukusanyaji wa mapato kwa upande wa Zanzibar na kuvuka lengo la ukusanyaji. Katika kipindi cha Julai hadi Disemba Mamlaka ilijiwekea lengo la kukusanya Tshs. 91,917.2 kupitia vianzio vyake vya kodi za ndani na kodi za forodha. Hadi kufikia Disemba Mamlaka imekusanya TSHS. 101,287.37 ambazo ni sawa asilimia 110. Mapato halisi ya kipindi cha Julai hadi Disemba kwa mwaka wa fedha 2016/2017 pamoja na ulinganisho wa mapato kwa kipindi cha Julai hadi Desemba,2015 utaonehswa katika Jadweli la hapo chini kama ifuatavyo:

Makusanyo katika kipindi Julai hadi Disemba, 2016

IDARA	**LENGO**	**MAPATO HALISI**	**ASILIMIA**
KODI ZA NDANI	34,768.9	38,540.9	108
FORODHA	57,148.3	62,746.4	110
JUMLA	**91,917.2**	**101,287.37**	**110**

CHANZO: TRA

Jadweli linalofuata chini linaonesha hali halisi ya makusanyo kwa TRA Zanzibar katika kipindi cha Julai hadi Disemba, 2015.

IDARA	LENGO	MAPATO HALISI	ASILIMIA
KODI ZA NDANI	30,644.0	30,590.5	99.8
FORODHA	56,321.8	44,786.5	89.2
JUMLA	**86,965.7**	**75,377.0**	**86.7**

CHANZO: TRA

Pamoja na mafinikio makubwa kwa TRA kuvuka lengo walilojiwekea katika kipindi cha miezi sita, lakini bado juhudi za ziada zinahitajika kwani wafanyabiashara wasiokuwa waaminifu wapo na wanatumia mbinu mbali mbali za kukwepa kulipa kodi hasa kwa mizigo inayoingizwa kupitia bandari ya Zanzibar. Tunaamini kuwa endapo kutakuwa na mikakati imara na uwadilifu kwa watendaji wetu mapato tunayokusanya yataongezeka kwa silimia kubwa zaidi.

Kuna ujanja unaotumiwa na baadhi ya wafanyabiashara wajanja kupitisha mizigo yao katika bandari ya Zanzibar na kuwatumia baadhi ya watendaji wa taasisi za Serikali wasiokuwa waadilifu kwa madai kuwa bidhaa hizo si kwa ajili ya biashara bali ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Zipo taarifa kuwa ujanja huu huwa unafanyika kupitisha mizigo bila ya kulipa kodi katika bandari yetu. Kamati inaitaka Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikiana na TRA kuwafatilia wafanyabiashara wajanja wa namna hii ambao wanarudisha maendeleo ya Serikali na wananchi kwa ujumla, na watakapobainika walipishwe kodi kwa kipindi chote ambacho wamekwepa kulipa kodi na hatua nyengine za kisheria zichukuliwe dhidi yao.

Naomba kuchukuwa nafasi hii kupitia Baraza lako tukufu kuwahikishia wananchi kuwa, mapato yote yanayokusanywa Zanzibar kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) yanaingia katika Mfuko wa Hazina wa Zanzibar na yanatumika kwa ajili ya Zanzibar. Kwahivyo, wananchi waondoe kasumba kuwa mapato haya yanakusanywa na kupelekwa Tanzania Bara.

CHANGAMOTO

Pamoja na mafanikio yanayoonekana kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania, lakini bado Bodi inakabiliwa na Changamoto zifuatazo:

(a) Zaidi ya asilimia 60 ya mapato ya TRA Zanzibar yanatokana na kodi inayotokana na Biashara ya Kimataifa. Hata hivyo, biashara ya Kimataifa haiaminiki kwa asilimia kubwa, mtikisiko wowte kwenye mtiririko wa biashara ya kimataifa utakaosababishwa na matatizo yoyote yakiwemo ya uchumi, kisiasa na kijamii yanaweza kuleta athari kubwa katika ukusanyaji wa mapato ya TRA.
(b) Mamlaka inapoweka udhibiti mkubwa kupitia Idara ya Forodha, ili kuhakikisha kodi zinalipwa ipasavyo, wadau wa uchumi wanalalamika kuwa Idara inacheleweshe utoaji wa mizigo na inaweka mazingira magumu kwa wafanyabiashara na wawekezaji, na iwapo Idara itaelemea kwenye ufanikishaji wadau katika uchumi pia wanalalamika Idara inavujisha mapato ya Serikali na kuhatarisha usalama wa nchi na watumiaji wa bidhaa.
(c) Mwamko wa kulipa kodi kwa hiari ni mdogo.
(d) Kuwepo kwa tatizo la ukwepaji kodi kwa makusudi au kutumia mapungufu ya Sheria zilizopo.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. TRA kwa kushirikiana na Shirika la Bandari la Zanzibar waangalie utaratibu mzuri ili kupunguza msongamano wa makontena bandarini ili iwe kivutio kwa Kampuni za meli kushawishika kuendelea kuitumia bandari ya Zanzibar katika kuleta mizigo.

2. TRA ihakikishe inafanya uhakiki wa taarifa za wafanyabiashara mara kwa mara katika mfumo wa usajili wa walipakodi.

3. TRA ishirikiane na Wizara ya Fedha na Mipango ya Zanzibar ili kuifahamu mizigo yote inayoingia Zanzibar ambayo inatumika kwa miradi ya maendeleo ili kuwabaini wafanyabiashara wajanja wanaopitisha bidhaa zao kwa mgongo huo.

4. TRA iimarishe mahusiano na sekta binafsi kwa kupokea na kuyafanyia kazi maoni, ushauri na mapendekezo kwa lengo la kuimarisha ukusanyaji wa mapato na kushajihisha ulipaji kodi kwa hiari.

BENKI YA WATU WA ZANZIBAR (PBZ)

Kamati yetu imeridhishwa na utendaji wa Benki ya Watu wa Zanzibar kwa juhudi kubwa walioifanya katika kuhakikisha kuwa mtaji wa Benki unaongezeka na idadi ya wateja inaongezeka. Samba samba na hilo, uimarikaji huo wa Benki unaenda sambamba na kufungua matawi ya Benki katika maeneo mbali mbali ya Zanzibar na Tanzania Bara, jambo ambalo limepelekea kuitangaza Benki na kuongeza wateja wanaotumia Benki hiyo. Kwa ujumla, Benki inayo matawi takribani kumi na moja kati ya hayo saba yapo Zanzibar ambayo ni Malindi,Chake Chake, Forodhani, Mwanakwerekwe , Mkoani, Wete na Mlandege na manne yapo Tanzania Bara mabayo ni Tawi la Kariakoo, Dar es Salam, Tazara na Mtwara, na Benki inampango wa kufungua matawi mengine ya Benki katika Mikoa mbali mbali ya Tanzania Bara.

Aidha, Kamati inatoa pongezi za dhati kwa Serikali kwa kukubali kusamehe gawio la faida ya Benki kwa Serikali (dividend), kwa lengo la kuimarisha mtaji wa Benki. Vile vile, Kamati inatoa pongezi kwa Benki kuongeza mashine za ATM ikiwemo katika eneo la Baraza la Wawakilishi ambapo kwa kipindi kirefu wajumbe walikuwa wakiomba kufungiwa mashine hiyo katika eneo la Afisi ya Baraza.

CHANGAMOTO

Pamoja na uimarikaji wa Benki, lakini bado Benki ya Watu wa Zanzibar inakabiliwa na Changamoto zifuatazo:

(a) Kutokuwepo kwa jengo la kutosha kwa ajili ya Afisi za Benki jambo ambalo linapelekea kukodi katika maeneo mengi kwa ajili ya shughuli za Benki.
(b) Baadhi ya wateja wanaokopa Benki kushindwa kulipa kwa wakati.
(c) Baadhi ya Sheria ambazo maudhui yake huendana na shughuli zinazofanywa na Benki kama vile Transfer of Property Decree kupitwa na wakati.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kwakuwa Benki inamiliki kiwanja kilichopo Mazizini, Benki ijipange kuanza ujenzi wa jengo jipya litakaloendana na mazingiza ya kisasa kwa ajili ya kutoa huduma za kibenki.

2. Sheria Transfer of Property Decree ifanyiwe marekebisho ili iendane na wakati tulionao.

3. Benki iweke mikakati bora ili iweze kuwadhibiti wanaojaribu kukwepa kulipa madeni yao ili waweze kulipa kwa wakati.

4. Benki iangalie uwezekano wa kulitumia soko la Afrika Mashariki badala ya kuangalia soko la ndani tu.

SHIRIKA LA BIMA LA ZANZIBAR

Kamati inalipongeza Shirika la Bima la Zanzibar kwa namna linavyofanya kazi na kuweza kuingia katika soko la ushindani ndani ya nchi. Shirika linalo jengo lake hapa Zanziba ambalo linatumika kama Makao Makuu ya Shirika, lakini vile vile limeanzisha matawi katika Mikoa mbali mbali ya Tanzania Bara ikiwemo Dar-es- Salam, Mwanza, Mbeya, Dodoma na Arusha.

Maendeleo ya Shirika la BIMA la Zanzibar kwa miaka mitano iliyopita, ukusanyaji wa ada za Bima na Madai, yanaoneshwa katika Jadweli la hapa chini kama ifuatavyo:

MWAKA	**2011**	**2012**	**2013**	**2014**	**2015**
MAPATO	9,600,000,000	10,500,000,000	13,000,000,000	18,308,000,000	20,200,000,000
MADAI	4,000,000,000	4,075,000,000	4,000,000,000	6,495,000,000	7,515,000,000

CHANZO: SHIRIKA LA BIMA LA ZANZIBAR

Hata hivyo, Shirika linakabiliwa na changamoto ya Afisi kwa upande wa Pemba lakini eneo la ujenzi wa Afisi tayari limeshapatikana na Shirika lipo tayari wakati wowote kuanza ujenzi baada ya taratibu kukamilika.Tunaiomba sana Serikali kuhakikisha eneo hili la ujenzi wa Afisi ya Shirika la Bima Pemba lililopo Chake Chake linapatiwa hatimiliki na Lease Certificate kutoka Wizara ya Ardhi kwani wenzetu wa Shirika la Bima wapo tayari kuanza kwa ujenzi wakati wowote.

Kamati yetu inatoa pongezi kwa Bwana Said Salum Bakhresa kwa kuendelea kuliunga mkono Shirika la Bima la Zanzibar kwa kukata Bima zake zote katika Shirika hili, jambo hili limefanya pia kuzidi kuimarika kwa Shirika la Bima. Tunaomba wafanyabiashara na wawekezaji mbali mbali walitumie Shirika la Bima katika kuikatia Bima miradi yao.

Pamoja na kuwepo kwa ushindani mkubwa wa kuwepo Mashirika ya Bima Tanzania, lakini Shirika la Bima la Zanzibar ni moja ya Mashirika ya umma ambayo yanaweza kupigiwa mfano kwa namna ya uwendeshaji wa shughuli zake kwani limeweza kuingia katika ushindani mkubwa wa kibiashara na linafanya kazi zake vizuri. Uimarikaji huu wa Shirika usingelipatikana kama si jitihada za Serikali katika kuliunga mkono Shirika hili.

CHANGAMOTO

Pamoja na uimarikaji wa Shirika lakini bado Shirika la Bima la Zanzibar linakabiliwa na Changamoto zifuatazo:

(a) Kukosekana kwa hatimiliki na lease certificate ya eneo la ujenzi wa Afisi ya Shirika la Bima la Zanzibar lililopo Chake Chake – Pemba.

(b) Uelewa mdogo kwa wananchi juu ya umuhimu wa kukata Bima.

(c) Kutokukatiwa Bima kwa miradi ya Serikali kwa Shirika la Bima la Zanzibar kwa lengo la kuifanya miradi kuwa katika usalama zaidi ikwemo miradi ZSFF na mengineyo.

(d) Kuwepo kwa mtandao unaochapisha Bima feki, jambo ambalo linasababisha kurudisha nyuma maendeleo ya Shirika.

(e) Baadhi ya wateja kuunguza vyombo vyao au kuharibu mali zao zilizokatiwa Bima kwa makusudi kwa lengo la kupatiwa fidia ya chombo kipya.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Serikali iharakishe kupatikana kwa hatimiliki na lease certificate ya eneo la ujenzi wa Afisi ya Shirika la Bima – Pemba ili ujenzi uanze haraka.

2. Jitihada za kutoa elimu kwa wananchi ziongezeke ikiwemo kutoa matangazo katika vyombo mbali mbali juu ya umuhimu wa kukata Bima.

3. Serikali ihakikishe kuwa vyombo vya Serikali vinakatiwa Bima katika Shirika la Bima la Zanzibar na Miradi yote ya Serikali ambayo inahitaji kukatiwa Bima basi Bima hizo zikatwe kupitia Shirika la Bima la Zanzibar.

4. Shirika la Bima na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) kwa kushirikiana na vikosi vya ulinzi iwatafute wote wanaohusika na kuchapisha Bima feki, na watakapowagundua hatua kali za kisheria zichukuliwe dhidi yao, sambamba na kutumika kwa soft ware itakayowezesha kugundua stika zisizo halali.

5. Shirika liwe makini sana wakati wa kulipa fidia za mali zilizoharibika ikiwemo vyombo vya moto kwani wapo wateja wengine wasiokuwa waaminifu ambao hufanya vitendo hivyo makusudi.

6. Shirika liangalie uwezekano wa kutafuta soko la Afrika Mashariki ili kulitangaza Shirika ndani na nje ya nchi.

7. Shirika liwe angalifu sana kwa mawakala na madalali wanaofanya kazi za Shirika, na isisite kuchukuwa hatua zinazofaa kwa watakaobainika kwenda kinyume na makubaliano ya Shirika.

MFUKO WA HIFADHI YA JAMII (ZSSF)

Kamati yetu inaipongeza sana Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kwa kuamua kuja na marekebisho ya Sheria Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ambayo yatapelekea kwa kiasi kikubwa kuimarisha uhai wa Mfuko. Ni wazi kuwa kwa wanachama wanaojiunga na Mfuko huu hasa watumishi wa umma hawawezi kujua umuhimu wa Mfuko huu mpaka pale watapafikia umri wa kustaafu. Tunawaomba sana nyinyi waheshimiwa wajumbe wa Baraza hili pamoja na wananchi wote waliopo ndani na nje ya nchi mjiunge katika Mfuko huu, kwani marekebisho ya Sheria yaliyofanywa sasa hivi kila mwananchi ataweza kujiunga katika Mfuko huu.

Miradi ya uwekezaji ni moja ya maeneo ambayo yanaweza kuimarisha maendeleo ya Mfuko, sote tutakuwa mashuhuda katika kipindi hiki ZSSF inaendelea kuwekeza katika miradi mbali mbali hapa nchini, miradi ambayo tayari imekamilika ni pamoja na ujenzi wa viwanja vya kufurahisha watoto Kariakoo – Unguja na Tibirinzi – Pemba, ujenzi wa mnara wa Mapinduzi Square – Kisonge, na miradi ambayo inaendelea ni pamoja na ujenzi wa nyumba za makaazi – Mbweni, ujenzi wa jumba la treni – Darajani na sasa hivi ipo katika hatua za maandalizi ya kuanza ujenzi wa jengo la biashara (shoping moll) – Michenzani.

Miradi yote hiyo endapo kutakuwa na usimamizi madhubuti itaimarisha sana maendeleo ya Mfuko kwa lengo la kutoa huduma bora zaidi kwa wanachama wake. Hata hivyo, Kamati yetu inasisitiza kuwa ZSSF jukumu lake la msingi ni kutoa huduma kwa wanachama wake na sio kufanya shughuli za uwekezaji, kwahivyo uwekezaji ufanywe ni moja tu ya nyenzo za kuimarisha Mfuko na sio kazi ya msingi ya Mfuko.

Suala la ukataji wa Bima kwa miradi ya Mfuko ni jambo muhimu sana ili kuwa na uhakika wa matumizi ya miradi hiyo kwa kipindi kirefu, lakini Kamati yetu inasikitishwa sana kwa ZSFF hadi sasa miradi mingi inayoisimamia bado haijakatiwa Bima. Kwasasa hivi ni mradi wa viwanja vya waoto Tibirinzi – Pemba na Mnara wa Mapinduzi Squre ndio iliyokatiwa Bima.

CHANGAMOTO

Pamoja na maendeleo hayo Mfuko lakini bado zipo changamoto zinazoukabili Mfuko kama hivi ifuatavyo:

(a) Baadhi ya waajiri wa sekta binafsi kushindwa kuwasilisha michango ya waajiriwa kwa Mfuko.

(b) Elimu ya kujiunga na Mfuko bado ni ndogo kwa wananchi hasa katika sekta isiyo rasmi.

(c) Muitikio wa wananchi wa Pemba katika kutumia kiwanja cha kufurahisha watoto Pemba bado ni mdogo sana.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Uongozi wa Mfuko uhakikishe unasimamia Sheria ya Mfuko ipasavyo ili kila anayestahiki kutoa michango aiwasilishe kwa wakati.

2. Mfuko uhakikishe mafao ya wastaafu yanapatikana kwa wakati mara tu pale wanapostaafu ili kupunguza malalamiko ya wanachama ya ucheleweshwaji wa mafao yao baada ya kustaafu.

3. ZSSF ihakikishe inasimamia vizuri miradi yake ya uwekezaji ili fedha za wanachama zinazotumika zirudi katika Mfuko na Mfuko uweze kujiendesha vizuri.

4. Elimu ya kujiunga na Mfuko kwa wananchi bado inahitajika hasa kwa watu wa sekta binafsi na wajasiriamali ambao bado hawajakuwa na mwamko mkubwa wa kujiunga na Mfuko licha ya kuanzishwa kwa Mfuko wa hiari.

5. Kuwe na usimamizi mkubwa sana kwa miradi ya uwekezaji ili kuhakikisha kuwa mapato yanakusanywa vizuri bila ya kuwa na uvujaji wa aina yoyote wa mapato yanayoingia.

6. Hatua kali za kinidhamu na kisheria zichukuliwe kwa mtu au mtumishi yeyote wa Mfuko atakaebainika kutumia vibaya miradi ya Mfuko.

7. ZSSF isimamie vizuri sana miradi yake hasa ya viwanja vya kufurahisha watoto ili iweze kutumika kwa muda mrefu sambamba na kukatiwa Bima. Kwani hadi sasa hivi ni miradi miwili tu ya ZSSF ambayo imekatiwa Bima (Mnara wa Mapinduzi Square na Viwanja vya Tibirinzi – Pemba)

8. Mfuko uanzishe programu maalumu kwa upande wa Pemba ili kuweza kuwashahijisha wananchi kukitumia kiwanja cha watoto - Tibirinzi.

9. Mfuko uhakikishe kuwa miradi yote ambayo inaendelea na ujenzi imalizike kwa wakati ili Mfuko usitumie gharama za ziada zaidi ya zile zilizokubaliwa awali.

10. Mfuko ukae pamoja na Wizara ya Kilimo na kuangalia ni namna gani wanaweza kuwekeza katika eneo lililopo Makurunge Bagamoyo.

11. Wizara isisimamie kikamilifu ili kuhakikisha kuwa miradi ya Mfuko inakatiwa Bima katika Shirika la Bima la Zanzibar.

MFUKO WA BARABARA

Kwa mujibu wa Sheria ya Mfuko wa Barabara Namba 2 ya 2001 kazi kuu ya Mfuko ni kufanya matengenezo ya barabara baada ya kujengwa. Katika utekelezaji wa jukumu hili, Mfuko hushirikiana na Wizara ya inayohusika na Usafirishaji (kwa barabara kuu) na Halmashauri (kwa barabara ndogo ndogo) ambapo taasisi mbili hizi hufanya mchakato wote wa kutafuta mkandarasi na kuingia mikataba nao na hatimaye Mfuko hufanya malipo kwa mujibu wa mkataba husika.

Kamati yetu imebaini kuwa, bado uongozi na uwendeshaji wa Mfuko haujakaa vizuri jambo ambalo linapelekea malalamiko makubwa kwa uongozi wa Mfuko na Wizara ya Mawasiliano. Kamati inashauri kuwa ipo haja ya kufanya mapitio juu ya uongozi na uwendeshaji wa shughuli za Mfuko ili kunazisha chombo maalumu ambacho kitahusika na usimamizi mzima wa shughuli za uwendeshaji wa Mfuko huu jambo hili litapelekea kuleta ufanisi mzuri wa utekelezaji wa kazi za Mfuko na kuondoa mivutano iliyopo baina ya Mfuko wa Barabara na Wizara ya Mawasiliano.

CHANGAMOTO

Mfuko unakabiliwa na changamoto zifuatazo:

(a) Tatizo la upatikanaji wa fedha kwa wakati.

(b) Mfuko kutoshirikishwa katika mchakato wa ujenzi wa barabara na badala yake umeonekana kazi yake ni kutoa fedha za ujenzi tu.

(c) Mahitaji ya matengenezo ya barabara yamekuwa makubwa ikilinganishwa na uwezo wa Mfuko.

(d) Kutokuwa na chombo maalumu ambacho kinasimamia mchakato mzima wa shughuli za ujenzi wa barabara jambo ambalo hupelekea mivutano baina ya Mfuko na Wizara zinazohusika na ujenzi wa barabara.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Wizara ihakikishe kuwa fedha zinazopatikana kupitia Mfuko wa Barabara ziwasilsihwe kwa wakati kulingana na mahitaji ya Mfuko.

2. Wizara kwa kushirikiana na vyombo vya dola, ihakikishe kuwa vyombo vyote vya moto vinavyotembea barabarani vimekatiwa leseni ya barabara ili kuongeza mapato ya Mfuko.

3. Wizara iangalie uwezekano wa kubakiza (retention) japo asilimia 10% ya makusanyo yake kwa ajili ya uwendeshaji mzuri wa shughuli za Mfuko.

4. Sheria ya Mfuko wa Barabara Namba 2 ya 2001 ifanyiwe marekebisho ili iendane na wakati kulingana na mahitaji yaliyopo.

5. Kwakuwa Mfuko ni mdau mkubwa katika ujenzi wa barabara, Serikali ihakikishe kuwa Mfuko unashirikishwa katika hatua zote za ujenzi wa barabara.

6. Kianzishwe chombo maalumu ambacho kitakuwa na maamuzi juu ya mchakato mzima wa ujenzi wa barabara ili kuondoa mivutano iliyopo Baina ya Mfuko na Wizara ya Mawasiliano.

7. Kamati inaitaka Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikiana na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ifanye ukaguzi juu ya thamani halisi ya fedha (value for maney) Tshs, 250,000,000/- zilizotumika kwa ajili ya mchanga uliomwagwa katika barabara ya Fuoni baada ya kukamilika kwa ujenzi wa barabara hiyo.

MAMLAKA YA UWEKEZAJI NA VITEGA UCHUMI (ZIPA)

Kwa ajili ya kurahisisha shughuli za uwekezaji nchini, Serikali katika mwaka 2004 kwa mujibu wa Sheria iliyopitishwa na Baraza la Wawakilishi ilianzisha Mamlaka ya Uwekezaji na Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA). Katika kushahijisha uwekezaji nchini, kwa makusudi Serikali iliamua kutangaza maeneo huru ya uwekezaji ambapo kwa Unguja ni eneo la Fumba na kwa upande wa Pemba ni eneo la Micheweni. Kuanzishwa kwa Mamlaka na kutangazwa kwa maeneo huru ni moja ya malengo ya Serikali kuwavutia wawekezaji nchini. Hata hivyo, kuwepo kwa Mamlaka na kutangazwa maeneo huru ni suala moja lakini kuwepo kwa miundombini ni suala jengine ambalo ni muhimu sana katika kuwavutia wawekezaji katika maeneo hayo.

Yapo mafanikio ambayo yameonekana kutokana na kuanzishwa kwa Mamlaka na kutangazwa kwa maeneo huru, ambapo ipo miradi mbali mbali ambayo tayari imeshapata idhini na vibali vya uwekezaji. Kati ya miradi hiyo ipo miradi ambayo imeshakamilika na ipo miradi ambayo inaendelea na ujenzi. Miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana kutokana na kuanzishwa kwa Mamlaka na kutangaza maeneo huru ni kama hivi ifuatavyo:

MRADI WA NYUMBA ZA BIASHARA – FUMBA UPTOWN LIVING LIMITED

Kamati inatoa pongezi kwa muwekezaji mzalendo Ndugu Bakhresa kwa kuamuwa kuwekeza katika maeneo mbali mbali katika mji wa Zanzibar ikiwemo kujenga mji wa kisasa katika eneo la Fumba. Kamati yetu ilifanya ziara katika eneo hili ambapo ilielezwa kuwa jumla ya hekta 90 zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha mradi ambapo nyumba mbali mbali zitajengwa na kuuzwa kwa watu wa ndani na nje ya nchi. Hadi Kamati yetu inatembelea katika eneo hilo, jumla ya nyumba 100 zimeanza kujengwa. Vile vile, ujenzi wa barabara kuu na za ndani zenye jumla ya kilimita 30 umeshafanyika ndani ya mji huo.

CHANGAMOTO

Changamoto zinazoikabili mradi huu

(a) Kuchelewa kuunganishwa umeme katika eneo la mradi. Tayari Kampuni imeshawasiliana na Shirila la Umeme Zanzibar (ZECO) na kuwapatia makisio ya mahitaji ya umeme katika eneo hilo na muwekezaji yuko tayari kulipia gharama hizo.

(b) Kuchelewa kuunganishwa kwa maji katika eneo la mradi. Tayari muwekezaji ameshawasiliana na Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) na kuwasilisha mahitaji ya maji katika eneo hilo.

(c) Ujenzi holela unaofanywa na wananchi katika maeneo yanayoendelezwa.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) ifanye haraka kuvuta umeme katika eneo hilo ili kuwatia moyo wawekezaji.
2. Mamlaka ya maji Zanzibar (ZAWA) iharakisha kufikisha maji katika eneo hilo.
3. ZIPA kwa kushirikiana na Afisi ya Mkuu wa Wilaya husika isimamie na kuchukuwa hatua kwa wanaovamia katika maeneo hayo.

MRADI WA MJI MDOGO WA NYAMANZI

Mradi wa mji mdogo wa Nyamanzi (Fumba Town Development Project) unatekelezwa ndani ya maeneo huru ya kiuchumi Fumba. Kulingana na mpango mkuu wa mradi, katika mradi huu jumla ya nyumba elfu moja na mia nne (1400) zitajengwa. Ujenzi wa nyumba hizo utakuwa ni katika mfumo wa nyumba za chini, nyumba za roshani moja hadi sita ambapo utekelezaji wake utakuwa na awamu nne.

Vile vile, kutakuwa na uwekezaji katika huduma za kijamii kama vile hospitali, viwanja vya michezo, vyuo vya elimu ya juu pamoja na huduma nyengine. Wanahisa wa Kampuni hii ni raia wa Ujerumani na Ubegiji.

CHANGAMOTO

1. Matakwa ya mradi kama huu unahitaji Sheria na Kanuni zinazowezesha wawekezaji kufanya biashara kwa wepesi. Tayari kuna Sheria ya Condominium Act ya 2010 lakini bado Sheria hii haijaanza kutekelezwa.

2. Kukosekana kwa utaratibu uliowazi wa kisheria utakaowawezesha wamiliki wa nyumba zitakazouzwa kwa miradi ya aina hii kupata warka zao kutoka kwa Waziri anaesimamia Ardhi.

3. Upatikanaji wa umeme wa uhakika na wa kutosha katika maeneo ya Fumba.

4. Dhana ya ujenzi wa nyumba za biashara bado ni ngeni katika sehemu nyingi za Afrika ya Mashariki ukiondoa Kenya, jambo hili linapelekea kuwepo kwa malalamiko mengi kutoka kwa wananchi.

MRADI WA UJENZI WA CHUMBA VYA CHINI YA BAHARI

Kamati yetu ilifanya ziara na kuona mradi wa ujenzi wa chumba cha chini ya bahari kilichopo Pemba, Kamati inawapongeza wawekezaji wa chumba hiki, lakini vile vile imefurahi kwa taarifa kuwa asilimia 80 ya wafanyakazi katika Hoteli yake ni wazalendo katika kazi zote za utaalamu na zisizokuwa za utaalamu.

Tunaomba sana Serikali ihakikishe inasimamia suala la ajira katika Hoteli za Zanzibar kama alivyofanya muwekezaji huyo.

Jambo la kufurahisha zaidi, ni pale Kamati yetu ilipopata taarifa kuwa wawekezaji hawa wanayo nia ya kujenga vyumba vyengine vinne vya chini ya bahari katika eneo la Pemba, maombi hayo tayari yapo ZIPA na yanafanyiwa kazi.

Tunaiomba sana ZIPA, kwa kufuata taratibu zilizopo kisheria maombi hayo ya wawekezaji yazingatiwe kwa mujibu wa Sheria na kwa wakati ili kuwapa moyo wawekezaji wanaokuja nchini.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Serikali kupitia Wizara ya Ardhi ianze utekelezaji wa Sheria ya Condominium Act ya 2010.
2. ZIPA na Wizara ya inayosimamia masuala ya Ardhi kwa kushirikiana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali iangalie uwezekano wa kisheria wa kupatiwa umiliki wa nyumba kwa mtu atayenunua nyumba zitakazouzwa kwa miradi ya aina hii.

3. Shirika la umeme kuharakisha uandaaji wa mpango wa matumizi ya umeme katika neno la Fumba.

MAENEO HURU YA MICHEWENI

Kamati wakati ikitekeleza majukumu yake ilifanya ziara ya maeneo huru ya Micheweni – Pemba. Lengo la Serikali kutenga eneo hili ni kuvutia wawekezaji katika kisiwa cha Pemba. ZIPA bado inalojukumu la kuyatangaza maeneo haya ili yaendelezwe kwa shughuli za uwekezaji, kwani hadi sasa hivi bado maeneo haya hayajaanza kutumika kwa hughuli hizo. Tunaamini kuwa endapo maeneo haya yatapata wawekezaji uchumi kwa upande wa Pemba utaimarika na Zanzibar kwa ujumla.

CHANGAMOTO

1. Ukosefu wa miundombinu kama vile barabara, umeme na maji katika maeneo huru.

2. Uharibifu wa mazingira unaosababishwa na ukataji wa matufali ya mawe.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Serikali kupitia ZIPA iweke miundombinu kwa jili ya kuwavutia wawekezaji katika maeneo hayo.

2. ZIPA kwa kushirikiana na Serikali za Mikoa na Wilaya iweke utaratibu maalumu kwa wananchi wanaokata matufali ya mawe ili kunusuru maeneo hayo na uharibifu wa mazingira.

UWEKEZAJI KATIKA HOTELI YA BWAWANI

Kamati ilipata taarifa kuwa Serikali imempa muwekezaji ili kuwekeza katika Hoeli ya Bwawani kwa lengo la kuifanya Hoteli iwe na mazingira ya kisasa ili iweze kuwavutia watalii na kuongeza mapato ya nchi. Kwa masikitiko makubwa sana tokea kutolewa samani na vitu vilivyokuwemo ndani ya Hoteli, ujenzi huu umesita kwa muda mrefu.

Tunaiomba sana Serikali ikamalishe taratibu na makubaliano na muwekezaji ili ujenzi huu uanze haraka kwani jengo hili lipo katikati ya mji na likiendelea kukaa kama lilivyo litaleta sura mbaya kwa mji wetu wa Zanzibar.

Kwa ujumla, umuhimu wa kuwepo kwa ZIPA kwa kiasi kikubwa umeonekana, lakini pamoja na kuwepo kwa mafanikio makubwa yaliyopatikana kutokana na kuanzishwa kwa Mamlaka hii

Zanzibar kwa ajili ya kurahisisha shughuli za uwekezaji nchini, bado kumekuwa na malalamiko makubwa kwa baadhi ya wananchi na wawekezaji kuwa Mamlaka hii kwa upande mwengine imekuwa ni kikwazo cha shughuli za uwekezaji nchini. Malalamiko haya yanatokana na ucheleweshwaji mkubwa wa majibu ya kukubaliwa au kukataliwa kwa miradi ya uwekezaji. Kwahivyo, katika Mamlaka hii inaonekana bado kuna tatizo aidha la kiutawala au kiutendaji.

Hata hivyo, katika kutekeleza majukumu yake, Mamlaka inakabiliwa na changamoto kubwa ya uhaba wa bajeti kwa ajili ya kuendesha shughuli za Mamlaka.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaitaka Mamlaka kuhahakikisha kuwa inasimamia kuendelea kufanyakazi kwa kituo cha One stop Center ili kurahisisha mchakato mzima wa shughuli za uwekezaji nchini.

2. Kwakuwa suala la uwekezaji linagusa sekta zote za Serikali, Kamati inaitaka Mamlaka kuwa na mashirikiano mazuri na Taasisi za Serikali.

3. Mamlaka kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, iangalie namna ya kutafuta wawekezaji kwa ajili ya kuendeleza eneo RAZABA – Bagamoyo.

4. Mamlaka ihakikishe kuwa, muwekezaji yeyote aliyetimiza masharti ya uwekezaji Zanzibar, anapatiwa kibali kwa wakati ili kuvutia wawekezaji wengine nchini na kuondosha usumbufu wa njoo leo, njoo kesho, njoo keshokutwa, mara Mkurugenzi hayupo.

5. Mamlaka inapoabaini kuwepo kwa wawekezaji wasiokuwa waaminifu, ihahakishe inatoa taarifa haraka iwezekanavyo kwa vyombo vinavyostahiki kwa ajili ya kuchukuliwa hatua zinazofaa.

6. Wizara ya fedha iongez ruzuku kwa Mamlaka, kwani ruzuku inayopata sasa hivi ukilinganisha na mahitaji ya Mamlaka bado ni ndogo sana.

7. Serikali kupitia Wizara ya fedha na kwa kushirikiana na Mamlaka, iharakishe kuweka miundombinu ya barabara, umeme na maji katika maeneo huru ya Micheweni ili kuvutia wawekezaji kisiwani Pemba.

8. Mamlaka kwa kushirikiana na Afisi za Mikoa na Halmshauri zidhibiti uharabifu wa mazingira unaoendelea kufanyika katika maeneo huru ya Micheweni hasa ukataji mawe kwa ajili ya kutengeneza matufali.

9. Kamati inaitaka Mamlaka kuwa na uwazi na uharaka pale yanapoletwa maombi ya Miradi ya uwekezaji kwa kuharakisha majibu ya waleta maombi ili kuondoa malalamiko kwa waombaji na kuondoa dhana za urasimu zilizojengeka kwa wananchi.

OFISI KUU PEMBA

Katika utekelezaji wa malengo yake iliyojipangia Wizara ya Fedha na Mipango Ofisi kuu Pemba ilipanga kukusanya jumla ya Tshs. 55,000,000 kama ni mapato kutoka katika vianzio vyake mbali mbali. Katika kipindi cha Julai hadi Disemba Ofisi iliweza kukusanya jumla ya Tshs. 12,257,500/- sawa na asilimia 22.27 ya bajeti iliyojipangia. Kamati inaipongeza Wizara kwa hatua nzuri ya ukusanyaji wa mapato, lakini bado tunaamini kuwa walipakodi wajanja wanaojaribu kukwepa kodi bado wapo, kwahivyo jitihada zichukuliwe ili kuwabaini watu hao na kuziba mianya hiyo ili mapato yazidi kuimarika.

Kwa upande wa matumizi, katika kipindi cha Julai hadi Disemba Afisi iliweza kupatiwa jumla ya Tshs. 134,109,000/- kati ya 137,836,900/- zilizopangwa ambazo ni sawa na asilimia 97.30 kwa nusu mwaka ikilinganishwa na bajeti ya mwaka.

Kamati imebaini kuwa Pemba bado kuna tatizo kubwa sana la matumizi ya fedha za umma yasiyofuata Sheria na Kanuni zilizopo hasa katika suala za ununuzi wa mali za umma, kwani katika Taasisi nyingi za Pemba hakuna wataalamu wakutosha katika fani za uhasibi na ununuzi na hivyo kupelekea kwa baadhi ya Taasisi wahasibu au washika fedha waliopo ndio wanakuwa maafisa ununuzi na hivyo kupelekea upotevu wa fedha za umma kwa kutokufuatwa taratibu za ununuzi wa mali za umma.

Changamoto zinazoikabili Afisi kuu Pemba ni kama ifuatavyo:

(a) Kukosekana kwa jengo linalokidhi mahitaji kulingana na majukumu ya Afisi.

(b) Uhaba wa wataalamu katika fani ya uhasibu, ununuzi na ukaguzi.

(c) Taratibu za manunuzi kutokufatwa ipasavyo kwa mujibu wa Sheria.

(d) Uvujaji mkubwa wa mapato kutokana na kuwepo kwa bandari bubu nyingi na maeneo yasiyo rasmi ya kupitisha mizigo.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Wizara ihakikishe jengo jipya la Wizara linaloendelea kujengwa katika eneo la Gombani linamalizika kwa wakati ili liondoe changamoto ya uhaba wa Afisi.

2. Serikali itoe vipaombele vya ajira kwa wahasibu na maafisa wanunuzi ili kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za umma kwa upande wa Pemba.

3. Wizara, kupitia Idara ya Uhakikimali, ihakikishe kuwa taratibu zote manunuzi zinafuatwa kwa mujibu wa Sheria, na hatua za kinidhamu zichukuliwe kwa mtumishi yeyote atakayebainika kwenda kinyume na Sheria au taratibu zilizopo kisheria.

4. TRA na ZRB ianzishe mpango maalumu wa kuhakikisha kuwa wanadhibiti tatizo la uvujaji wa mapato kisiwani – Pemba na Zanzibar kwa ujumla.

5. Serikali itoe mafunzo kwa maafisa wa ununuzi wa Unguja na Pemba ili kuwajengea maadili ya kufuata taratibu za ununuzi wa mali za umma

SEHEMU YA TATU
WIZARA YA BIASHARA, VIWANDA NA MASOKO

Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko imeundwa na Idara nne, Shirika moja, Baraza moja pamoja na Ofisi Kuu Pemba kama ifuatavyo:-

I. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.
II. Idara ya Biashara na Ukuzaji Masoko.
III. Idara ya Maendeleo ya Viwanda na Ukuzaji Ujasiriamali.
IV. Idara ya Uwendeshaji na Utumishi.
V. Afisi Kuu – Pemba.
VI. Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC).
VII. Baraza la Kusimamia Mfumo wa Utoaji Leseni.
VIII. Shirika la Viwango la Zanzibar (ZBS)
IX. Baraza la Taifa la Biashara

UTEKELEZAJI WA BAJETI

Kamati iliarifiwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara ilitengewa jumla ya shilingi 6884.4 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida. Kwa kipindi cha Julai - Disemba jumla ya shilingi 3,993.6 milioni zilitengwa kwa matumizi hayo ambapo fedha zilizopatikana kwa matumizi hayo ni shilingi 1,759.9 sawa na asilimia 44.

Kwa upande wa makusanyo, Wizara ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 371.23 milioni kwa mwaka 2016/2017. Hadi kufikia Disemba 2016, jumla ya shilingi 130.598 milioni zilikusanywa sawa na asilimia 35 ya malengo ya mwaka.

Katika suala la miradi ya maendeleo, jumla ya shilingi 500 milioni zilikadiriwa kutumiwa na Wizara kwa mwaka 2016/2017 kwa ajili ya mradi wa kukondoesha masuala ya biashara chini ya ufadhili wa UNDP. Hadi kufikia Disemba 2016, fedha hizo bado hazijapatikana.

PROGRAMU KUU YA VIWANGO NA TATHMINI YA UBORA

Programu hii imetengewa kiasi cha Tshs. 1,529,000,000/- kwa jili ya utekelezaji wa majuku yake. Ambapo programu hii inasimamiwa na **TAASISI YA VIWANGO ZANZIBAR (ZBS).**

Kwa kipindi cha Julai - Disemba 2016, Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) iliendelea na majukumu yake makuu ya kuweka viwango na kusimamia ubora wa bidhaa na huduma nchini, iwe zinazozalishwa au kuingizwa nchini kutoka nje ya nchi na kuimarisha biashara katika soko la ndani pamoja na biashara za kimataifa. Aidha, Kamati iliarifiwa kuwa mchakato wa ununuzi wa vifaa vya maabara ya umeme unaendelea vizuri ambapo inategemewa kuanza rasmi April 2017. Kadhalika, hatua za uanzishaji wa maabara ya mafuta na nishati unaendelea.

ZBS imeanzisha utaratibu wa ukaguzi wa bidhaa nje ya nchi kabla ya kuingia ndani ya nchi (PVOC), ukaguzi huu utasaidia sana mrundikano wa bidhaa ambazo zinasubiri kufanyiwa ukaguzi wa ubora bandarini. Jambo hilo sio jipya kwa ZBS kwani yapo mashirika mengi yanayofanyakazi zinazolingana na ZBS ikiwemo TBS yanatumia utaratibu huu. Lakini Kamati

yetu bado haijaridhika na asilimia za mgao wa mapato baina ya ZBS na mawakala wa ukaguzi waliopo nje ya nchi, kwani kwa mujibu wa makubaliano wakala anapata 70% na ZBS 30% kwa kila bidhaa au chombo kinachokaguliwa. Kamati inaitaka ZBS utakapomaliza mkataba huu ifanye upya tathmini ya mgao wa mapato kwani inaonekana Shirika linakosa fedha nyingi.

Kupitia Shirika ZBS, Zanzibar imepata uwanachama mwangalizi wa Shirika la Viwango la Afrika (ARSO), jambo ambalo linatoa fursa kwa ZBS kupatiwa mafunzo yanayohusiana na utendaji wao wa kila siku pamoja na kujitangaza ndani na nje ya Afrika Mashariki. Kwa nafasi hii ya mwanachama mwangalizi, Zanzibar haina fursa yoyote katika kufanya maamuzi ya shirika hilo ingawa ina jukumu la kulipia USD 80 kwa mwaka.

Kamati yetu ilipata kutembelea Afisi za Shirika la Ubora la Tanzania (TBS) na kuona hatua kubwa zilizofikiwa za kimaendeleo kwa Shirika hili ikiwemo pamoja na kuwepo kwa maabara zenye mashine za kisasa kwa ajili ya kupima ubora wa bidhaa mbali mbali. Vile vile imeanzisha Afisi zake katika baadhi ya Mikoa ya Tanzania ambayo inapitisha bidhaa kwa wingi. Maendeleo haya hayakufikiwa isipokuwa ni kupatiwa bajeti za kutosha pamoja na kuwa na wataalamu ambao hutumia taaluma zao kwa ajili ya maendeleo ya Shirika.

CHANGAMOTO

1. Sheria ya biashara ya Zanzibar haijaweka wazi mamlaka ya ZBS katika kutekeleza majukumu yake ya kudhibiti ubora wa bidhaa zinazozalishwa nchini.

2. Uhaba wa wataalmu, maabara, vifa vya maabara na vitendea kazi jambo ambalo linapelekea nafasi za kitaalamu kukaimiwa na watendaji wachache waliopo na kupunguza ufanisi wa kazi.

3. Tatizo la upatikanaji wa fedha kwa wakati.

4. Uelewa mdogo kwa wazalishaji, wafanyabiashara na watumiaji juu ya umuhimu wa viwango na ubora wa bidhaa.

5. Baadhi ya wajasiriamali waliolewa umuhimu wa viwango na ubora wanashindwa kuwasilisha maombi ya uthibiti ubora kutokana na gharama zilizopo.

6. Kutokana na uchanga wa taasisi hii, fedha nyingi zinahitajika kwa ajili ya uanzishwaji wa maabara na ununuzi wa mashine na vitendea kazi vya kila siku vya maabara hizo.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Marekebisho ya sheria ya biashara yafanyike ili kuipatia fursa taasisi ya viwango Zanzibar (ZBS) kufanya ukaguzi wa bidhaa zote zinazozalishwa ndani na zinazoingia nchini.
2. Kamati inaishauri ZBS kubuni miradi mbali mbali ili kukabiliana na tatizo kubwa la uhaba wa vifaa linalowakabili.
3. Kamati inaitaka Wizara kupitia ZBS wazitumie ipasavyo fursa zinazopatikana kwenye shirika la viwango la Afrika.

4. Wizara itafute suluhisho la upungufu wa wataalamu unaoikabili ZBS ili kuweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

5. Utaratibu wa PVOC uangaliwe upya kwani hali ya sasa ya mgao wa 30% ya mapato kwa Shirika na 70% kwa wakala inayoendesha ukaguzi huo hairidhishi kutokana na Zanzibar kupata kiwango kidogo sana cha fedha.

6. ZBS ibuni miradi ndani ya Shirika ili kuweza kupata ufadhili wa majengo ya maabara pamoja na mashine na vifaa vyengine vya maabara.

7. Serikali iwe na mpango wa kuanzisha maabara ya ZBS Pemba kwani kumekuwa na malalamiko kwa waingizaji na wazalishaji bidhaa kuchelewa kwa majibu ya sample kwa ZBS.

8. Serikali iweke bajeti maalumu ya wajasiriamli ili iweze kuwasaidia katika kuthibitisha ubora ubora wa bidhaa zao.

PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA VIWANDA NA UJASIRIAMALI NCHINI

Programu hii imetengewa kiasi cha Tshs. 354,425,000/- kwa jili ya utekelezaji wa majuku yake. Lengo kuu la Programu hii ni kusimamia Ukuzaji wa Viwanda na Maendeleo ya Wajasiriamali. Kwa kuwa Zanzibar inaelekea katika kuwekeza kwenye uchumi wa Viwanda, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa Wizara ishirikiane na taasisi zinazohusika ili kuweka mazingira bora ya kisheria na kisera ili kuwavutia wawekezaji katika sekta ya viwanda nchini.

UIMARISHAJI WA VIWANDA NCHINI

Kamati ilitaka kujuwa kuhusu jitihada za uimarishwaji wa viwanda nchini zimefikia wapi. Kamati ilielezwa kuwa kwa kiasi kikubwa viwanda vidogo vidogo vimeimarika nchini ambapo hadi sasa jumla ya viwanda 2050 vinafanya kazi nchini. Hata hivyo, idadi kubwa ya viwanda hivyo ni vidogo vidogo. Kwa upande wa Serikali, ni kiwanda kimoja tu ambacho inakimiliki nacho ni kiwanda cha makonyo kilichopo Pemba. Jitihada za Serikali zinaendelea kuhakikisha kuwa inatafuta wawekezaji au kuimarisha mashirikiano na taasisi binafsi ili kuimarisha sekta ya viwanda nchini.

Katika kufanikisha hilo, Wizara ipo katika mpango wa kuandaa Sera ya uwendelezaji wa viwanda pamoja na kuanda Sheria ya uwendelezaji wa viwanda ili kuweza kuwavutia wawekezaji nchini.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Wizara ishirikiane na Mamlaka ya Uwekezaji (ZIPA) katika kuimarisha suala la uwekezaji wa viwanda.

2. Sera na Sheria zifanywe haraka ili ziweze kutumika na ziweze kuwavutia wawekezaji.

3. Ili tuweze kuimarisha viwanda vya ndani, unahitajika uzalishaji mkubwa wa bidhaa ili ziweze kutosheleza mahitaji ya viwanda vya ndani.

4. Serikali zifanye mazungumzo ili suala la usajili wa Viwanda libaki katika Serikali ya Zanzibar badala ya viwanda kusajiliwa Tanzania Bara.

Katika kufuatilia utekelezaji wa Programu hii, Kamati ilifanya ziara katika kiwanda cha Sukari - Mahonda.

KIWANDA CHA SUKARI – MAHONDA

Kamati ilifanya ziara na kupokea taarifa kuhusu utekelezaji wa shughuli za kiwanda hicho na iliiarifiwa kwamba, uzalishaji wa sukari chini ya mwekezaji mpya kutoka India ulianza mwezi Julai 2016 ambapo hadi wakati Kamati ilipotembelea kiwanda hicho jumla ya tani 4517 zilizalishwa. Bidhaa nyengine zinazozalishwa kiwandani hapo ni pamoja na spiriti na umeme upatao mega wati 1700. Kimsingi, Kamati imeridhishwa na kasi uzalishaji wa kiwanda hicho kwani wamefanikiwa kuitumia malighafi yote inayopatikana (miwa) na kuwa na mahitaji ya ziada ili kuendelea na uzalishaji kwa ufanisi.

Ni ukweli usiopingika kuwa, maendeleo ya kiwanda hichi yatategemea kwa kiasi kikubwa mashirikiano mazuri baina Serikali na mwekezaji kwa kila mmoja kati yao kutekeleza wajibu wake. Kwa upande wa Serikali ni kuhakikisha mazingira mazuri ya uzalishaji kwa kuweka miundombinu inayostahiki, sera na sheria zinazokubalika na kuondoa urasimu kwenye mambo ya uwekezaji. Kwa upande mwengine, mwekezaji ana wajibu wa kufuata sera na sheria zinazoongoza uwekezaji, kuchangia pato la taifa kwa kulipa kodi zote zilizowekwa na Serikali.

CHANGAMOTO

1. Uhaba wa ardhi ya uzalishaji wa mali ghafi ya kiwanda hicho (miwa).
2. Uvamizi wa eneo la shamba unaofanywa na wananchi kwa ujenzi wa makaazi na matumizi ya ardhi hiyo kwa kilimo mbadala.
3. Uchomaji wa moto unaofanywa mara kwa mara na wakulima wa mazao mengine hususan pale wanapohitaji kusafisha mashamba yao.
4. Ufinyu wa makaazi kwa watendaji wa kiwanda hicho kwani nyumba nyingi za kiwanda bado zinatumiwa na watu na hazipo chini ya kiwanda.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kwa nia ya kukiimarisha zaidi kiwanda hichi, Serikali inapaswa kuwapatia ardhi ya kutosha wawekezaji hawa ili waweze kuzalisha miwa ya kutosha na hatimaye kulifikia lengo la uzalishaji wa kutosheleza soko la ndani na kusafirisha nje ya nchi kwa maslahi ya Taifa.
2. Kamati inaiagiza Wizara kusimamia ipasavyo urejeshwaji wa nyumba za kiwanda ambazo zinatumika kwa shughuli mbali mbali kama makaazi ya watu wasiohusika ili zirudishwe kwenye mamlaka ya kiwanda na kuondoa usumbufu uliopo wa makaazi ya wafanyakazi.

KIWANDA CHA MAKONYO

Kamati ilitembelea kiwanda cha makonyo tarehe 02/11/2016 na kupata maelezo kuhusiana na uzalishaji wa kiwanda hicho. Katika ziara yake kiwandani hapo, Kamati ilibaini kuwepo kwa mali ghafi (makonyo ya karafuu) kwa kiwango kikubwa na kuarifiwa kuwa mali ghafi hiyo ilikuwa imerundikana kutokana na kusita kwa muda uzalishaji kutokana na kuharibika kwa mashine.

CHANGAMOTO

1. Gharama kubwa za umeme ambazo hupelekea kuongezeka kwa gharama za uzalishaji na hivyo kupelekea kutokidhi haja kwa bei za bidhaa za kiwanda hicho.

2. Uchakavu wa mashine ambazo zimetengenezwa tangu kiwanda kilipoanzishwa hadi sasa hivi.

3. Kutopatikana kwa spea za mashine zilizoharibika kutokana na kutumia teknolojia ya zamani ambayo haipo tena duniani. Hivyo, Mafundi wa kiwanda hicho hulazimika kufanya kazi ya ziada kila inapotokea kuharibika kwa mashine ili kukihami kiwanda hicho cha pekee hapa Zanzibar kiweze kuendelea na uzalishaji.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaitaka Wizara kupeleka maombi maalum kwa Serikali juu ya haja ya kukifanyia matengenezo makubwa kiwanda hicho ili kwenda sambamba na teknolojia ya uzalishaji duniani na kukidhi matakwa ya soko la ndani.
2. Wizara ichukuwe hatua za makusudi za kudhibiti uuzwaji wa mafuta ya makonyo kwa watu wasiowaaminifu ambao huyanunua mafuta hayo kwa kiwango kikubwa na kuyachakachua na baadae kuyauza nje ya nchi kwa njia zisizo halali. Kuendelea kwa biashara hii haramu kutapelekea kushuka hadhi ya mafuta yetu kwenye soko la Kimataifa na kuathiri uchumi wa Taifa letu.
3. Ipo haja kwa Serikali kukiangalia kwa jicho la huruma kiwanda hicho na kukiandalia mpango maalum wa kupata umeme nafuu utakaowezesha kufanyika uzalishaji kwa gharama zinazokubalika. Utafiti unapaswa kufanywa juu ya njia ipi ya uzalishaji wa umeme utakiwezesha kiwada hicho kufikia malengo yake (ya kuzalisha bidhaa bora kwa bei nafuu) ili kuweza kuhimili ushindani wa biashara uliopo kwenye soko.
4. Kiwanda kiendelee kujitangaza kupitia vyombo mbali mbali ndani na nje ya nchi ili iweze kuwa na soko kubwa la bidhaa zake.

MAENDELEO YA SHUGHULI ZA UJASIRIAMALI

Kamati yetu inatoa pongezi za dhati kwa Serikali kwa jitihada zake za kuwaunga mkono wajasariamali nchini. Katika kutekeleza kazi zake, Kamati ilikutana na baadhi ya wajasiriamali kwa upande wa Unguja na Pemba ili kusikiliza changamoto zao kwa lengo la kuzifikisha Serikalini na kuchukuliwa hatua muafaka ili tuzidi kuimarisha shughuli za wajasiriamali.

CHANGAMOTO

(a) Ukosefu wa utaalamu kwa wajasiriamali.

(b) Ukosefu wa vitendea kazi.

(c) Uhaba wa mitaji ya kuendesha shughuli za wajasiriamali.

(d) Kutokuwepo kwa viwanda vya kusarifu mazao, jambo linapelekea bidhaa zinazozalishwa kuharibika.

(e) Ushindani mkubwa wa soko la bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali wetu ikilinganishwa na bidhaa kama hizo zinazoingizwa nchini.

(f) Uharibifu wa mazao ya wajasiriamali ambayo husababishwa na wafugaji au kuchomwa moto mashamba.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaitaka Wizara kuendelea kutoa taaluma kwa wajasiriamali ili waweze kuzalisha bidhaa zenye ubora na ziweze kuingia katika soko la ndani na nje.

2. Serikali iongeze bajeti ya wajasiriamali kwa kutoa mikopo ya kutosha, kwani wajasiriamali wanachangia pato la Taifa kwa kiasi kikubwa.

3. Wizara ya biashara ifanye tathmini ya bidhaa zinazozalishwa kwa wingi nchini, na kuona ni namna gani wanaweza kulinda bidhaa za ndani ikilinganishwa na bidhaa zinazoingizwa kwa lengo la kuwainua na kuwatia moyo wazalishaji wa ndani.

4. Wizara iandae maonyesho mbali mbali ili wajasiriamali wapate kuonesha bidhaa zao na kuzitangaza ili waongeze masoko ya bidhaa zinazozalishwa hapa nchini.

5. Kutokana na uzalishaji mkubwa wa bidhaa za kilimo nchini ambazo huzalishwa na wakulima pamoja na wajasiriamali, kuna haja ya kuwa na kiwanda cha kusafiri mazao kwa upande wa Pemba na Unguja.

6. Kutokana na kubainika kwa kemikali zinazotokana na dawa ya mbu inayopulizwa majumbani kwenye bidhaa za viungo (organic spices) zilizosafirishwa nchini Ujerumani, Kamati inaitaka Wizara ya Biashara kuhakikisha kwamba bidhaa zote za viungo zinazozalishwa nchini ziwasilishwe ZBS kwa ajili ya ukaguzi kabla ya kusafirishwa nje ya nchi ili kulinda hadhi ya bidhaa hizo na jina la Zanzibar kwenye soko la kimataifa.

PROGRAMU KUU YA UKUZAJI NA UENDESHAJI WA BIASHARA

Programu hii imetengewa jumla ya Tshs. 2,994,570/- kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zake. Program hii inasimamia Uendeshaji wa Biashara na Ukuzaji wa Masoko na Usafirishaji, Ushindani Halali wa Kibiashara na Kumlinda Mtumiaji na Urahisishaji Biashara na Ukuzaji Biashara za Ndani. Katika kutekeleza Programu hii Wizara imefanya shughuli mbali mbali ikiwemo pamoja na ukaguzi wa mezani katika maeneo mbali mbali , kuimarisha masoko, ukaguzi wa biashara na maghala, n.k.

TATIZO LA MASOKO NCHINI

Kwakuwa Wizara hii inahusika na masuala ya masoko, Kamati ilitaka kujuwa kuhusu maendeleo ya masoko kwa bidhaa zinazozalishwa ndani ya nchi. Kamati ilielezwa kuwa, ni kweli katika suala la masoko zipo kasoro nyingi kwasababu kitengo hiki cha masoko hakipo wazi katika muundo wa Wizara, jambo ambalo linapelekea pia usimamizi wake kutokuwa mzuri. Hata hivyo, Wizara ilipeleka ombi la kuanzishwa Idara ya masoko ili sekta ya masoko iweze kusimamiwa vizuri chini ya Idara husika.

Pamoja na kuwepo kwa mchakato huu wa kutaka kuanzishwa kwa Idara itakayaosimamia masoko nchini, lakini Wizara bado inalo jukumu la kuhakikisha kuwa soko la bidhaa za ndani linaimarika kwa kuwa na mikakati na mipango madhubuti ili kuwalinda wazalisahi wa ndani

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

Wizara kwa kushirikiana na Taasisi zinazohusika iwe na mpango maalumu wa kuimarisha soko la bidhaa zinazozalishwa ndani.

SOKO KATIKA ZAO LAMWANI

Kamati ilitaka kujuwa pia kuhusu jitahada za Wizara kulifanya zao la mwani kuwa ni zao la kitaifa ili wakulima wa zao hilo wapate soko la uhakika zimefikia wapi. Kamati ilielezwa kuwa, bado Wizara inaendelea kufanya utafiti hasa tukiangalia uzalishaji wa mwani bado haujakuwa mkubwa sana, kuna Kamati maalum ambayo imeundwa inayofuatilia biashara ya zao hili kulifanya la kitaifa na baadae itawasilisha taarifa yake kwa Waziri.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

Wizara iendelee kutoa ushirikiano mkubwa kwa wakulima wa mwani kwani bei ya zao hili bado ipo chini kulinganisha na soko la mwani duniani.

UBORA WA MIZANI ZINAZOTUMIWA NA WAFANYABIASHARA NCHINI

Kamati ilitaka kujuwa kuhusu ubora wa mezani zinazotumiwa na wafanyabiashara kwani kumekuwa na udanganyifu mkubwa kwa mezani hizo. Kamati ilielezwa kuwa, Wizara kupitia taasisi zake inafanya ukaguzi wa ubora wa mezani mara kwa mara katika maeneo mbali mbali ndani ya nchi, hata hivyo kumekuwa na baadhi ya wafanyabiashara wadanganyifu ambao huziondosha makusudi uhalisia wa mezani kwa kupunguza kipimo halisi cha mezani husika. Pamoja na jitihada hizo, Wizara imepiga marufuku matumizi ya mezani za springi kwani mezani hizi ni kwa ajili ya matumizi ya nyumbani tu na sio kwa matumizi ya biashara.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Wizara iongeze nguvu ya ukaguzi wa mezani kwani kumekuwa na mlalamiko mengi kwa wananchi juu ya udanganyifu wa vipimo halisi vya mezani.

2. Mezani zinazoingia nchini zianze kukaguliwa kabla ya kuanza kutumika ili kubaini ubora wake mapema.

3. Wizara ichukuwe hatua kwa watakaobainika kufanya udanganyifu katika mezani zao.

4. Wizara ifanye ukaguzi wa mara kwa mara kwa bidhaa ambazo zimeshapekiwa ili kujiridhisha kuwa zinafika uhalisia wa ujazo wake, kwani tayari kuna malalamiko kuwa baadhi ya vipolo vyenye ujazo wa kilo 25 na 50 huwa hazifikii ujazo huo.

MAGHALA YA SERIKALI

Kamati ilitaka kujuwa kuhusu hali ya maghala ya Serikali yaliyopo chini ya Wizara ya Biashara, Kamati ilielezwa kuwa, maghala ya Serikali mengine yameuzwa na mengine yamekodishwa na baadhi yapo mikononi mwa Serikali. Vile vile, Kamati ilitaka kupatiwa orodha ya maghala ya Serikali ambapo katika orodha hiyo ilionesha kuwa yapo baadhi ya magahala yaliyokodishwa yameshamaliza muda wake wa ukodishwa. Kamati ikaiagiza Wizara kufanya mapitio upya ya mikataba ya ukodishwaji wa maghala lakini baadae Kamati ikaelezwa kuwa maghala yote yapo ndani ya kipindi cha mkataba. Vile vile, Kamati yetu ilipopitia orodha hiyo imebaini kuwa watu ambao wamekodishwa maghala hayo baadhi yao kuna utofauti wa jina la aliyekodishwa na mtu halisi anayetumia ghala. Kamati ina wasi wasi kuwa wanaokodishwa maghala haya wanayakodisha tena kwa watu wengine (sub contract).

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaitaka Wizara kuyafanya tathmini kwa maghala yote yaliyo chini yake ili kufahamu hali yake na kubuni mbinu sahihi za matumizi yake.
2. Wizara ihahakikishe mtu anayekodishwa ghala ndiye anapaswa kutumia ghala hilo, akishindwa kulitumia alirudishe.
3. Utaratibu wa ukodishaji wa maghala uwe wa uwazi.
4. Wizara ifanye mapitio ya bei zinazokodishwa maghala na ihakikishe kuwa bei ya ghala iendane na hali ya ghala na sehemu lililopo ghala husika.
5. Wizara iandae mpango maalumu kupitia kodi zinazotokana na maghala, kuyafanyia matengenezo maghala yote ambayo hali yake ni mbaya

SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA (ZSTC)

Kwa mwaka wa fedha 2016/2017 shirika lilijiwekea malengo mbali mbali yakiwemo kutekeleza majukumu yake ya kila siku kama vile usimamizi na ununuzi wa zao la karafuu na kulisafirisha nje ya nchi. Kimsingi jumla ya tani 2,810 zilipangwa kununuliwa ambapo hadi kufikia 30 Disemba, 2016 jumla ya tani 2,056 za karafuu zilinunuliwa kutoka kwa wakulima ambazo ni sawa na asilimia 73 ya malengo ya mwaka.

Kwa upande wa usafirishaji, jumla ya tani 1,550 za karafuu kavu zenye thamani ya USD **11.8** milioni sawa na TZS 25.7 bilioni zilisafirishwa na kuuzwa nje ya nchi katika kipindi hicho.

Kamati inalipongeza Shirika la ZSTC kwa kuendelea kuifuata sera ya Serikali ya kununua karafuu kwa asilimia 80 ya bei ya kuuzia nje ya nchi. Hii ni faraja kubwa kwa wakulima wa zao hili hususan bei hiyo inapopanda kwenye soko la dunia na kwa Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kutokana na kupungua kwa uuzaji wa karafuu nje ya nchi kwa njia ya magendo. Ikizingatiwa kuwa ununuzi huu, baadhi ya wakati hasa katika kipindi kama hiki umekuwa ukifanywa na Shirika kwa hasara kwani bei ya karafuu nje imeshuka lakini bei ya kununua ndani bado ipo pale pale.

Ili kuzidisha udhibiti wa zao la karafuu, Kamati inakubaliana na suala zima la uwekwaji wa vizuwizi vya barabarani pamoja na ukaguzi wa mizigo inayosafirishwa baina ya sehemu moja na

nyengine, kwani imebainika kuwa baadhi ya watu hutumia usafiri wa barabara kuzisafirisha karafuu hadi kwenye bandari bubu na kuzisafirisha karafuu hizo nje ya nchi.
Kwa upande mwengine, Kamati inakemea suala la uuzaji wa karafuu za vikombe na kuitaka Serikali kupitia shirika la ZSTC kupiga marufuku biashara hii ambayo inachochea wizi wa karafuu mashambani.

Aidha, Kamati inatoa pongezi za dhati kwa Wizara kupitia shirika hili la ZSTC kwa kukamilisha awamu ya mwanzo ya branding ya karafuu za Zanzibar. Hii ni hatua muhimu ya kujitangaza na kudhibiti ubora wa karafuu zetu kwenye soko la kimataifa.

CHANGAMOTO

1. Kujitokeza kwa wimbi la uingizwaji wa karafuu kutoka Tanzania bara ni tishio kwa biashara ya karafuu za Zanzibar. Ingawa hadi sasa karafuu hizo kutoka maeneo ya Morogoro zimeigia nchini kwa kiwango kidogo ambacho hakioneshi athari ya moja kwa moja kwa nchi yetu, hatua za haraka zinahitaji kuchukuliwa ili kukomesha uingizwaji huo holela wa karafuu tukitilia maanani kuwa eneo la Tanzania bara ni kubwa na wana uwezo wa kuzalisha zaidi ya uzalishaji wetu. Aidha, hatua hizo zilenge kuilinda karafuu ya Zanzibar isichanganywe kwa njia za hadaa na karafuu nyengine jambo ambalo litaishusha hadhi ya karafuu yetu kwenye soko la dunia.

2. Katika upasishaji wa zao la karafuu, Kamati ilielezwa kuwa zaidi ya asilimia 90 ya karafuu zilizonunuliwa kwa kipindi cha Julai/Septemba 2016 zilikua ni za daraja la kwanza jambo ambalo kiuhalisia haliyumkiniki kutokana na mazingira ya uvunaji, uchambuzi na uanikaji wa karafuu kwa wakulima wetu. Kinachotia wasiwasi zaidi ni kwamba wasimamizi wa zao hilo ni Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko wakati wapasishaji wa karafuu ni Wizara ya Kilimo, Mliasili, Mifugo na Uvuvi.

3. Kutokuwepo mashine za kusafishia karafuu kisiwani Pemba na hivyo shirika kulazimika kuzisafirisha karafuu hadi Unguja ili kusafishwa na kusafirishwa nje ya nchi kwa mauzo jambo ambalo linazidisha gharama kwa Shirika.

4. Kuwepo kwa wanunuzi wa karafuu mbichi za kikombe, jambo ambalo linasababisha wizi wa karafuu kwenye mashamba.

5. Kushukua kwa bei ya karafuu katika soko la dunia kutokana na uzalishaji mkubwa wa karafuu kwa baadhi ya nchi.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaitaka Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kufanya utafiti wa kina juu ya karafuu zinazoingizwa kutoka Tanzania Bara na hatimaye kuweza kubaini athari zake kwa soko la karafuu za Zanzibar.

2. Kamati inaishauri Wizara kupitia Shirika la ZSTC kuajiri mtu wa kudumu wa Shirika ambae atakuwa ni mkaguzi wa zao la karafuu ili kuepusha mivutano baina ya wakaguzi wa Wizara ya Kilimo na watu wa Shirika.

3. Kamati inaitaka Wizara kupitia shirika la ZSTC kuweka mashine za kusafishia karafuu kisiwani Pemba ampako uzalishaji mkubwa wa karafuu hufanyika. Jambo ambalo litapunguza gharama na kuondoa mzunguuko usio wa lazima. Kwa mnasaba huo, karafuu ikitoka Pemba iwe tayari kwa kusafirishwa ni jambo la kusitikitisha sana kuwa hadi hii leo karafuu kwa upande wa Pemba zinasafishwa kwa kutumia machungio.

4. Katika suala zima la usimamizi na uendelezaji wa zao la karafuu, Kamati inashauri Wizara ya Biashara na Wizara ya Kilimo kuangalia namna bora ya kuchagua miche ya mikarafuu kabla ya upandaji wake. Pia, Wizara hizo zinapswa kufanya mazungumzo ya kitaalamu yatakayopelekea kupatikana kwa namna bora ya uoteshaji wa zao la karafuu. Kwani Kamati imebaini kuwa miche mingi inayotolewa kwa wakulima inakufa.

5. Serikali ipige marufuku na ihakikishe inasimamia uuzaji wa karafuu za kikombe ili kudhibiti wizi wa karafuu.

6. Shirika litoe taaluma kwa wakulima wa karafuu wanaotesha miche kwenye vitalu kwa ajili ya kuliuzia Shirika juu ya msimamo wa Shirika katika ununuzi wa miche hiyo ili kuondoa malalamiko ya wakulima kwa Shirika kukataa kununua miche yao.

7. Ili kuweza kuingia katika ushindani wa kimataifa na kuifanya karafuu ya Zanzibar iwe na hadhi ya kipekee, Shirika kupitia Wizara liharakishe kukamilika kwa branding ya karafuu ya Zanzibar.

8. Kamati inalitaka shirika la ZSTC kuandaa mipango madhubuti ya kuendeleza kilimo cha viungo (spices) kwani imebainika kuwa soko la bidhaa hizo ni kubwa duniani na hadi sasa Zanzibar hatujaitumia fursa hii kikamilifu.

BARAZA LA TAIFA LA BIASHARA LA ZANZIBAR

Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ilikutana na Baraza la Taifa la Biashara mnamo tarehe 09/11/2016 katika afisi zake zilizopo Forodhani mjini Zanzibar na kupokea taarifa ya utendaji wa kazi za Baraza hilo. Katika taarifa hiyo, Kamati iliarifiwa kuwa Baraza hilo lilianzishwa mwaka 2009 chini ya uenyekiti wa Rais wa Zanzibar wa wakati huo Mhe. Dkt. Aman Abeid Karume na katibu wake kuwa ni Katibu mkuu Kiongozi. Baraza linaundwa na wajumbe 26 ambapo wajumbe 14 wanatoka sekta ya umma na wajumbe 12 kutoka sekta binafsi.

CHANGAMOTO

1. Kutokuwa na wafanyakazi wa kudumu jambo ambalo linasababisha kuzorota kwa kazi za Baraza na kushuka kwa ufanisi.

2. Kukosekana kwa usafiri wa uhakika kwani gari inayotumika kwa shughuli za Baraza ni moja tu ambayo iko katika hali mbaya ya uchakavu.

3. Upungufu mkubwa wa vitendea kazi.

4. Sekta binafsi ambazo zilipaswa kuchangia uendeshaji wa shughuli za Baraza hazichangii na hivyo kuibebesha Serikali mzigo mzito.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Baraza lifanye mazungumzo na Wizara ya Utumishi wa Umma ili kuangalia namna ya kupatiwa wafanyakazi kutoka kwenye taasisi ambazo zina ongezeko la wafanyakazi.
2. Katika kukabiliana na upungufu mkubwa wa vitendea kazi, Kamati inalishauri Baraza kutumia fedha zake za matumizi ya kawaida (OC) ili kupunguza tatizo hilo hatua kwa hatua kwa kadri hali itakavyoruhusu.
3. Baraza liweke utaratibu maalumu wa kuchangia katika uendeshaji wa shughuli zake ili sekta zote mbili (sekta ya umma na sekta binafsi) zichangie gharama hizo ili,kuimarisha mfuko wa Baraza hilo.

BARAZA LA KUSIMAMIA MFUMO WA UTOAJI LESENI

Baraza la kusimamia mfumo wa utoaji leseni za biashara (Business Licensing Regulatory System Council) limeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Kusimamia Mfumo wa Utoaji Leseni Nam. 13 ya mwaka 2013 kwa madhumuni ya kusimamia mfumo wa utoaji leseni, vibali na ruhusa nyengine za uendeshaji wa biashara nchini. Baraza hili lina jumla ya Wajumbe13, 7 kati yao wanatoka kwenye sekta ya umma na 6 wanatoka sekta binafsi. Jukumu kubwa la Baraza ni kuweka mfumo wa aina moja wa utoaji wa leseni ambao utaondoa urasimu na utaratibu wa biashara moja kupewa leseni na mamlaka zaidi ya moja.

Kimsingi, mfumo uliopo wa utoaji wa leseni unakabiliwa na changamoto zifuatazo:

1. Baadhi ya biashara kupewa leseni zaidi ya moja na taasisi tofauti.
2. Baadhi ya leseni hutumika kama chanzo cha mapato na sio chombo cha kusimia na kuendeshea biashara.
3. Kuwepo na aina tofauti za leseni, vibali au ruhusa vya kuendesha biashara ambazo zote zina lengo moja (license, permit, authorization, classification, accreditation, certification).
4. Kuwepo kwa vyombo vingi vinavyotoa leseni bila ya kuwepo msimamizi (regulator) wa vyombo hivyo.
5. Baadhi ya leseni kutokuweka masharti ya kusimamia biashara wala kufanya ukaguzi.
6. Mfumo usio rafiki, una urasimu, unachukua muda, una gharama (cost of doing business) katika upatikanaji wa baadhi ya leseni.

Uundwaji wa Baraza hili unatarjiwa kuondoa kwa kiasi kikubwa mapungufu yaliyopo kwenye mfumo wa sasa yaliyoainishwa hapo juu.

UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA BARAZA

Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Baraza limetengewa jumla ya shilingi 232 milioni ambapo jumla ya shilingi 105.3 milioni kwa ajili ya mishahara, na shilingi 126.7 milioni kwa kazi za kawaida. Katika kipindi cha Oktoba/Disemba 2016, baraza lilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 50.714 milioni na kufanikiwa kuingiziwa shilingi 31.150 milioni sawa na asilimia 61.4 ya makadirio hayo.

Kwa upande wa miradi ya maendeleo, Baraza likiwa ni mdau wa programu maalum ya miaka mitatu inayofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) chini ya usimamizi wa Wizara ya Fedha na Mipango, liliandaa programu ya utekelezaji wa sheria ya kusimamia mfumo wa utoaji leseni ambao unahusisha uandaaji wa kanuni, ununuzi wa vifaa, uandaaji wa mpango

mkakati, utoaji wa mafunzo na matumizi ya mifumo ya kompyuta katika utendaji wa kila siku wa baraza yenye thamani ya USD 495,000.

CHANGAMOTO

Katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku, Baraza linakabiliwa na changamoto mbali mbali

1. Ufinyu wa bajeti unaopelekea Baraza kutotekeleza malengo yake kikamilifu.
2. Upungufu wa wa wataalamu hususan katika fani za uhasibu, uchumi na sheria.
3. Uelewa mdogo wa wafanyakazi wa mamlaka za utoaji leseni katika masuala ya usimamizi wa majukumu ya baraza.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kwa kuzingatia mifumo mbali mbali ya kodi iliyopo ulimwenguni, Baraza lichaguwe mfumo sahihi wa usimamizi wa leseni utakaokwenda sambamba na mazingira ya biashara ya nchi yetu ili kupunguza malalamiko kwa wafanya biashara.

2. Baraza lichukuwe hatua za makusudi za kukuza mashirikiano na taasisi za usimamizi wa leseni za Tanzania Bara kama TIRA ili kupata uzoefu zaidi hasa ikizingatiwa kwamba taasisi hizo zina uzoefu katika masuala haya.
   Aidha, Kamati inatoa wito kwa Baraza kutojikita kwenye taasisi za Serikali pekee bali liingie pia kwenye taasisi binafsi ili liwe na wigo mpana katika kutekeleza majukumu yake.

3. Kamati inalitaka Baraza kujitangaza kwa kutumia vyombo vya habari kama redio na TV ili liweze kutambulika kwa jamii.

4. Wizara ipeleke kibali maalumu kwa Wizara inayohusika na masuala ya Utumishi ili kuomba uhamisho kwa baadhi ya wafanyakazi waliomo katika Taasisi ambazo kuna ongezeko kubwa la wafanyakazi au kuajiri wafanyakazi wapya ili Baraza liweze kutekeleza kazi ipasavyo..

AFISI KUU PEMBA

Katika utekelezaji wa malengo yake iliyojipangia Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko Afisi kuu Pemba ilipanga kukusanya jumla ya Tshs. 15,000,000/- katika bajeti ya mwaka huu kama ni mapato kutoka katika vianzio vyake mbali mbali. Katika kipindi cha Julai hadi Disemba Afisi iliweza kukusanya jumla ya Tshs. 6,059,500/- sawa na asilimia 86.6 ya bajeti iliyojipangia. Kamati inataka Wizara kupitia Afisi kuu Pemba iongeze jitihada za ukusanyaji wa mapato kwani bado tunaamini kuwa yapo maeneo ya ukusanyaji wa mapato ambayo Wizara haijayafikia na pia wapo wajanja wanaojaribu kukwepa kodi.

Kwa upande wa matumizi, katika kipindi cha Julai hadi tarehe 04/Januari,2017 Afisi imeingiziwa Tshs. 131,253,700/- kwa ajili ya mishahara ambayo ni sawa na asilimia 60.99 ya kilichoombwa ikilinganishwa na bajeti ya mwaka na 86,430,000/- kwa ajili ya matumizi mengineyo ambazo ni sawa na asilimia 69.3 ya kilichoombwa ikilinganishwa na bajeti ya mwaka.

SEHEMU YA NNE
WIZARA YA KILIMO, MALIASILI, MIFUGO NA UVUVI

MUNDO WA WIZARA

Muundo wa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ni kama ifuatavyo:

I. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti
II. Idara ya Uwendeshaji na Utumishi
III. Idara ya Kilimo
IV. Idara ya Misitu na Maliasili zisizorejesheka
V. Idara ya umwagiliaji maji
VI. Idara ya uhakika wa Chakula na Lishe
VII. Idara ya Maendeleo ya Mifugo
VIII. Idara ya Maendeleo na Uvuvi
IX. Taasisi ya Utafiti wa Kilimo
X. Chuo cha Kilimo Kizimbani
XI. Ofisi Kuu Pemba

UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA KAMATI YALIYOTOKANA NA RIPOTI YA KAMATI YA MWAKA 2014/2015

Kamati katika kutekeleza kazi zake iliitaka Wizara kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa Maagizo ya Kamati yaliyotokana na Ripoti ya Kamati kwa mwaka wa 2014/2015. Kwa ujumla Kamati iliridhishwa kwa hatua zilizofanywa katika kutekeleza kwa baadhi ya maagizo na maoni ya Kamati. Isipokuwa Kamati yetu inaendelea kusisitiza katika maagizo yafuatayo:

Mradi wa ujenzi wa kituo cha usarifu wa mazao (Kizimbani)

Kamati imeridhishwa na jitihada za Serikali kupitia Wizara ya Kilimo kwa hatua iliyofikiwa ya ujenzi wa kituo cha usarifu wa mazao Kizimbani pamoja na changamoto ya upungufu wa vifaa kutokana na udanganyifu uliofanywa na Kampuni ya Kikorea iliyotakiwa kuleta vifaa vya kituo hicho.

Hatahivyo, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo kwa upande wake bado inayojukumu la kukamilisha ujenzi wa kiwanda hicho pamoja na kufunga mashine ili kiweze kufanya kazi zake, kwani sasa hivi kumekuwa na kilio kikubwa sana kwa wakulima na wajasiriamali kutokana na uzalishaji mkubwa wa bidhaa za kilimo ambazo zinakuja kwa msimu na hivyo zinapokaa muda mrefu kuharibika kutokana na kukosekana kwa kiwanda cha kusarifu mazao.

Tunaomba sana ujenzi wa kiwanda hiki ukamilike ili bidhaa zinazozalishwa ndani ziweze kusarifiwa na kuweza kutumika kwa matumzi mengine na pia kuongeza uzalishaji wa bidhaa kwa wakulima wetu.

Uwekwaji wa lami kwa barabara zilizojengwa chini ya Programu ya Uimarishaji miundombinu ya masoko (MIVARF)

Progaramu hii ya ujenzi wa barabara ilikuwa ni kwa kiwango cha kifusi, na maeneo mengi ya vijiji vya Unguja na Pemba yalifaidika na program hii. Kamati iliyopita iliagiza Wizara ya

Kilimo kwa Kushirikiana na Wizara inayohusika na Miundombinu kuziweka barabara hizi katika kiwango cha lami ili kuzifanya barabara hizi ziweze kutumika kwa muda mrefu lakini pia kupunguza athari ya vumbi inayoweza kuwapata watumiaji wa barabara hizi. Kwani sasa hivi tayari zipo barabara ambazo zimeshaanza kupata athari ya kukatika.

Kamati yetu inafahamu kuwa mahitaji ya ujenzi wa barabara ni makubwa kulinganisha na uwezo wa Mfuko wa Barabara, hata hivyo Kamati inaendelea kusisitiza juu ujenzi wa barabara hizi kwa kiwango cha lami ili ziweze kudumu kwa muda mrefu.

Gharama za umeme kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji maji

Kutokana na kupanda kwa gharama za umeme, kumekuwa na kilio kikubwa cha wakulima kuweza kulipia gharama hizo, lakini Kamati imejiridhisha kuwa endapo wakulima watapewa elimu ya kilimo bora na cha kitaalamu wataweza kupata mavuno mengi na wataweza kumudu gharama za umeme. Hata hivyo, Wizara iharakishe kumalizika kwa utafiti wa matumizi ya umeme wa nguvu za jua (Solar energy) ili kama uwezekano utakuwepo wa kutumia nishati hiyo, Serikali kupitia Wizara ianze mpango huo ili kuwapunguzia wakulima gharama za kilimo.

Ukarabati wa maghala ya chakula

Kamati imeridhishwa na jitihada za Serikali kupitia Wizara ya Kilimo kwa kuanzisha mpango maalumu wa ujenzi wa ghala la kitaifa ambapo taratibu za ujenzi huo tayari zimeshaanza na kwa sasa hivi mkandarasi kwa jili ya kuandaa mchoro ameshakamilisha kazi yake na wakati wowote zabuni itatangazwa kwa jili ya kuanza ujenzi huo.

UTEKELEZAJI WA BAJETI

Mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara imepangiwa kukusanya jumla ya **Tsh. 2,817,599,000** kutokana na vyanzo vyake tofauti vya mapato. Aidha, Wizara ya Kilimo Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa kipindi cha nusu mwaka (Julai – Disemba) ilikadiriwa kukusanya Tsh. 1,561,156,800 hadi kufikia mwezi wa Disemba imekusanya Tsh 1,347,112,109 sawa na asilimia 86.

Mwaka wa fedha 2016/17 Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi imeidhinishiwa kutumia jumla ya **Tsh. 48,977,300,000.** Kati ya fedha hizo **Tsh. 15,743,300,000** ni kwa ajili ya kazi za kawaida (**Tsh. 10,955,400** Mishahara, **Tsh. 4,236,400,000** matumizi ya kazi za kawaida na **Tsh. 551,500,000** ikiwa ni Ruzuku kwa ajili ya Chuo cha Kilimo Kizimbani. Kwa upande wa fedha za maendeleo Wizara imeidhinishiwa jumla ya TSh. **33,324,000,000** ambapo **Tsh**. **32,166,000,000** kutoka kwa washirika wa maendeleo na **Tsh. 1,068,000,000** ni kutoka SMZ.

Kwa kipindi cha Julai - Disemba Wizara imekadiriwa kutumia **Tsh. 9,080,730,096** (TSh. 5,625,979,590 ikiwa ni Mishahara, **TSh. 3,104,750,506** kwa kazi za kawaida na **TSh. 350,000,000** Ruzuku kwa Chuo cha Kilimo cha Kizimbani). Katika kipindi cha Julai - Disemba, 2016 Wizara imepatiwa **Tsh. 4,312,520,045** ambapo **Tsh. 5,625,979,590** kwa ajili ya mishahara sawa na asilimia 100. **Tsh. 2,204,317,040** kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 71 na **Tsh. 313,161,500** sawa na asilimia 89 ikiwa ni Ruzuku kwa ajili ya Chuo cha Kilimo Kizimbani.

Kwa upande wa fedha za maendeleo Wizara ilikadiriwa kutumia jumla ya **Tshs. 8,010,166,383** ambapo **Tshs. 7,666,280,223** kutoka kwa washirika wa maendeleo na **Tsh.567,378,228** kutoka SMZ. Hadi kufikia Disemba 30, Wizara imepata jumla ya **TSh. 3,553,572,332** ambapo (**Tsh.**

3,290,378,754 kutoka kwa washirika wa maendeleo sawa na asilimia 43 na **Tsh. 263,193,578** kutoka SMZ sawa na asilimia 46.

SEKTA YA KILIMO

Sekta hii inasimamiwa chini ya **Programu kuu ya Maendeleo ya Kilimo,** ambapo jumla ya Tshs. 6,615,744,000/- zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Programu hii. Kamati imeridhishwa na juhudi zinazochukuliwa na Serikali kupitia Wizara ya Kilimo ili kuhakikisha sekta ya kilimo inaimarika kwa kasi kubwa nchini, kwa lengo la kuinua kipato cha mkulima na uchumi wa nchi kwa ujumla. Kamati yetu inaunga mkono jitihada za Wizara ya Kilimo katika kuhakikisha kuwa Zanzibar inaimarika kwa kilimo hasa katika kilimo cha mpunga kwa kuwa na uzalishaji mkubwa wa bidhaa hiyo na kuacha kuagizia mchele nje ya nchi. Jitihada za Wizara zimeonekana kufanikiwa na tunaamini endapo kutakuwa na mashirikiano baina ya wananchi hasa wakulima na Serikali yao basi jambo hili litawezekana.

Zanzibar ina jumla ya hekta 8,521 za mashamba yanayoweza kutumika kwa kilimo cha umwagiliaji maji. Hadi sasa hivi hekta 800 tayari zinalimwa kwa kilimo cha umwagiliaji maji, jambo la kusikitisha maeneo ya kilimo kama vile mabonde ya Mwera valley na Mtwango tayari yapo katika hatari ya uvamizi, lakini vile vile kuna uvamizi mkubwa wa maeneo ya vianzio vya maji ambavyo hupeleka maji katika mabonde mbali mbali yanayolimwa mpunga na vianzio hivyo ni kama vile Kianga (chem chem), Mto Mwanakombo, Chaani, Kipange na Mwera Kinu Moshi,.

Mabadiliko ya tabia nchi ni moja ya changamoto kubwa sana iliyopelekea kupungua kwa kasi ya uzalishaji wa bidhaa za kilimo ikiwemo mpunga, jambo ambalo Serikali imelazimika kuimarisha huduma za kilimo kwa kuwa na kilimo cha umwagiliaji maji. Katika kuhakikisha hili, Wizara kwa jitihada zake imefanikiwa kupata wawekezaji katika sekta ya kilimo ambao wamekubali kuwekeza katika kilimo cha umwagiliaji maji. Miongoni mwa Kampuni zilizoleta maombi hayo ni Kampuni ya Netafim kutoka Israel na Kampuni Echelon SA kutoka Sychelles. Kampuni hizi tayari zimeshapata kibali kutoka ZIPA na kuanza kutekeleza kazi zake kwa kuwasilisha maandiko yao ya awali na kuanza mchakato wa uchambuzi yakinifu kwa kushirikiana na Serikali. Tunaomba sana Serikali iharakishe kuanza kwa miradi hii ya uwekezaji ili iwanufaishe wananchi wa Zanzibar.

Kamati inaipongeza sana Serikali kupitia Wizara ya Kilimo kwa kuanza kutoa elimu na kushajihisha wakulima kutumia mbinu za kilimo cha shadidi ambacho hutumia mbegu kidogo na maji ya wastani na mavuno yanakuwa makubwa. Wizara tayari imeshawashajihisha wakulima 1,110 (690 Unguja na 420 Pemba) wa mabonde ya umwagiliaji maji kutumia kilimo kilimo cha shadidi. Wajumbe wa Baraza hili watakuwa mashahidi kuwa, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Mhe. Balozi Seif Ali Iddi alikuwa mgeni rasmi katika uzinduzi wa kuvuna mpunga wa shadidi hivi karibuni na umeonekana ukulima wa aina hii utakuwa ni mkombozi kwa wakulima.

CHANGAMOTO

(a) Kuchelewa kwa upatikanaji wa pembejeo za kilimo.

(b) Mabadiliko ya hali ya hewa ambayo husababisha mvua zisizotabirika na vipindi virefu vya jua.

(c) Uvamizi katika mashamba ya mpunga na vianzio vya maji.

(d) Ubovu wa miundombinu ya umwagiliaji maji jambo hupelekea baadhi ya wakulima kukosa huduma hii ya umwagiliaji maji.

(e) Kuinama sana kwa nguzo za umeme zilizopita katika bonde la Cheju, jambo ambalo linahatarisha maisha ya wakulima wanaotumia bonde hilo.

(f) Elimu ndogo kwa wakulima juu ya mpango wa Wizara kununua pembejeo za kilimotanzania Bara jambo ambalo limepelekea malalamiko mengi kwa wakulima kwa Wizara kushindwa kununua pembejeo zao.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Wizara iwasiliane na wazabuni wanaoleta pembejeo za kilimo kuharakisha uletaji wa pembejeo hizo ili wakulima ziwafike kwa wakati.

2. Wizara kwa kushirikiana na masheha na Serikali za Wilaya ihakikishe kuwa mabonde yanayotumika kwa shughuli za kilimo na maeneo ya vianzio vya maji hayavamiwi.

3. Wizara iendelee na jitihada zake kutumia fedha zake za OC kwa kufanya ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji maji pale hali inaporuhusu ili huduma hii iwafikie wakulima wote katika maeneo yao.

4. Wizara iendelee kufuatilia ili kuhakikisha Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO) linafanya matengenezo ya nguzo za umeme zilizoinama katika bonde la Cheju.
5. Wizara itoe elimu kwa wakulima juu ya mpango wa Wizara kununua pembejeo za kilimo kutoka kwa wakulima ili kuondoa malalamiko yanwakulima.
6. Wizara itoe ushirikiano wa dhati kwa wawekezaji wote wanaowekeza au wanaokusudia kuwekeza kwenye sekta zinazosimamiwa na Wizara ya Kilimo.

7. Wizara ishajihishe wananchi kulima kilimo cha *spices* kwani kilimo hiki kimekuwa na soko kubwa ilimwenguni.

UTAMBUZI WA MASHAMBA YA SERIKALI

Kamati ilitaka kujuwa kuhusu kutambuliwa kwa mashamba ya Serikali yanayosimamiwa na Wizara ya Kilimo, kwani Kamati ilibaini kuwa yapo mashamba mengi ya Serikali ambayo hayajajulikana na hivyo yanatumiwa na watu binafsi kwa ajili ya shughuli zao binafsi na sio kwa masllahi ya wananchi.

Kamati ilielezwa kuwa, Wizara tayari imeshayatambua mashamba 5,057 kati ya mashamba 8,107 yaliyokabidhiwa na Serikali, kwa mnasaba huo bado mashamba 3,050 hayajatambuliwa na Wizara. Kamati yetu inaomba kutoa wito kwa Wajumbe wa Baraza hili na wananchi wote kwa ujumla pamoja na Masheha, Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa kuwa zoezi hili sio tu la Wizara ya Kilimo bali linahitaji mashirikiano ya hali ya juu kwani tunaamini kuwa ni sisi miongozi mwetu ndio tunaoyatumia mashamba haya na wanaoyatumia wanafahamika. Kwakweli zoezi hili litakuwa gumu sana endapo hakutakuwa na mashirikiano.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Serikali itamke rasmi kuwa yeyote iliyemiliki shamba la Serikli kinyume na utaratibu alirudishe Serikalini na itoe tamko kali kwa atakayekataa kulirudisha.

2. Wajumbe wa Baraza hili, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya pamoja na Masheha na wananchi watoe ushirikiano wa dhati kwa Wizara ili kuyatambua mashamba yaliyobaki na yaweze kutumika kwa maslahi ya wananchi.

3. Utaratibu wa ukodishwaji wa mashamba ya Serikali uwe wa wazi ili kuepuka malalamiko yaliyopo.

SEKTA YA UVUVI

Sekta hii inasimamiwa chini ya **Programu kuu ya Maendeleo ya Uvuvi,** ambapo jumla ya Tshs. 19,416,727/- zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Programu hii**.** Kama tunavyofahamu kuwa Zanzibar ni kisiwa ambacho kimezungukwa na rasilimali kubwa sana Bahari. Sekta ya Uvuvi ni moja ya sekta ambayo Serikali inategemea kupata mapato yatokanayo na sekta hii. Lakini bado mapato katika sekta ya uvuvi Zanzibar kulingana na rasilimali ya bahari tuliyonayo hayaridhishi na hayaendani na ukubwa wa rasilimali yetu. Kwa mfano; katika bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017 Makadirio ya bajeti katika sekta ya uvuvi ni Tshs. **1,000,949,000/-** katika pato la Taifa.

Kulingana na ukubwa wa rasilimali ya bahari tuliyonayo mchango wa Sekta ya uvuvi katika pato laTaifa bado ni mdogo sana. Hatahivyo, Kamati yetu inaipongeza Serikali kupitia Wizara hii kwa jitihada kubwa inazozifanya katika kuimarisha sekta ya uvuvi nchini kwa lengo la kuinua kipato cha wananchi na pato la Taifa. Miongoni mwa jitihada hizo na mpango wa Serikali kujenga soko la kisasa la samaki katika mtaa wa Malindi ambalo litaweka mazingira mazuri ya shughuli za uvuvi na kuweza kuwavutia wawekezaji. Lakini vile vile, Wizara tayari imeshapata muwekezaji katika sekta ya Uvuvi ambaye ni Kampuni ya Demko kutoka Ugiriki, fursa hizi za uwekezaji zitaimarisha sana sekta hii. Lakini vile vile, Kampuni nyengine mbili zimeshaleta maandiko ya awali (concept note) kwa ajili ya uwekezaji katika sekta ya uvuvi. Kampuni zenyewe ni Hongdong Investiments Co.ltd kutoka China na Yu Shian Group of Companies ambapo wenye Kampuni hiyo ni kutoka Taiwan, Thailand na Zanzibar.

Mpango wa Serikali katika kuimarisha sekta hii uwende sambamba na kutafuta wawekezaji katika kuanzisha viwanda vya kusarifu samaki ambapo kamati yetu imeshuhudia kuwa bidhaa ya samaki inaweza kutengezwa zaidi ya bidhaa 70 zinazotokana na samaki. Tunaamini kuwa jambo hili litawezekana endapo Serikali itaweka mazingira mazuri kwa ajili ya kuwavutia wawekezaji nchini.

Kamati yetu ilibahatika kukutana Wenyeviti wa Kamati za Uvuvi kwa Unguja na Pemba na kubadilishana mawazo juu ya mafanikio na changamoto zinazoikabili sekta ya uvuvi nchini. Kwa ujumla yapo mafanikio makubwa yaliyopatika hii ni kutokana na kuwepo kwa Sheria ya Uvuvi ya Zanzibar Namba 7 ya 2010 ambayo imesaidia sana katika kuweka masharti bora kwa ajili ya usimamizi mzuri wa matumizi ya rasilimali ya bahari yetu. Hata hivyo, zipo Changamoto zinazowakabili wavuvi katika pande zote mbili ambazo kwa ujumla changamoto hizo zinalingana. Kamati imebaini kuwa kuwepo kwa changamoto hizi kunasababishwa na ukuaji

mdogo wa sekta ya uvuvi, tunaamini kuwa endapo sekta hii itaimarika changamoto zote za wavuvi nazo zinaondoka. Tunaiomba sana Wizara iendelee kukaa karibu na wavuvi ili kuzijuwa changamoto zao na kujitahidi kuzipatia ufumbuzi.

CHANGAMOTO

(a) Kuwepo kwa uvuvi haramu nchini.

(b) Kutokuwepo kwa usimamizi wa kutosha katika madiko ya wavuvi.

(c) Kamati za wavuvi kushindwa kufanya kazi zao kwa mujibu wa Sheria kutokana na kuingiliwa katika majukumu yao wakati wanapotaka kufanya maamuzi.

(d) Uhaba wa vyombo vya doria za baharini.

(e) Uhaba wa elimu ya uhifadhi endelevu wa rasilimali ya bahari kwa wavuvi.

(f) Changamoto ya vyombo vya usafiri kwa wenyeviti wa kamati za uvuvi jambo linapelekea kushindwa kuyafikia maeneo mengi ya uvuvi.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Serikali ihakikishe inasimamia kuzuia uvuvi haramu unaofanywa na baadhi ya wavuvi, pamoja na kutafuta vyombo vya kutosha kwa ajili ya kufanya doria za baharini na kuwachuklia hatua za kisheria pale wanapoabainika.

2. Wizara iandae utaratibu maalumu wa usimamizi wa madiko kwani baadhi ya madiko yanaonekana hayatunzwi vizuri na yanatumika kinyume na malengo yaliyokusudiwa.

3. Wizara iwaunge mkono wenyeviti wa kamati za uvuvi kwa kuwa pamoja nao ili waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo pasi na kuingiliwa na watu wengine.

4. Wizara iendelee kutoa elimu kwa wavuvi ili wafahamu umuhimu wa kuwepo kwa maeneo ya uhifadhi baharini.

5. Wizara iharakishe kuwapatia vitambulishe wajumbe wa Kamati za uvuvi ili waweze kufanya kazi zao kwa kujiamini.

MAMLAKA YA UVUVI WA BAHARI KUU

Hii ni Taasisi ya Muungano ambayo inasimamiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzani, na mgao wa mapato yanayotokana na uvuvi wa bahari kuu yanagaiwa kwa SMZ, SMT na kwa Mamlaka kwa ajili ya uwendeshaji wa shughuli za Mamlaka. Serikali ya Zanzibar endapo itaweka miundombinu katika bandari zetu ili meli zinazovuwa katika bahari yetu ziweze kufikia bandarini, tutaweza kuingiza mapato mengi zaidi yanayotokana na uvuvi.

Kamati yetu inaitaka Wizara ya Kilimo kukaa pamoja naShirika la Bandari ili kuona ni namna gani bandari yetu inaweza kuwekwa miundombinu ambayo meli za uvuvi zitaweza kufikia bandarini hapo, kwa lengo la kuongeza mapato yatokanayo na uvuvi.

Vile vile Kamati inaomba sana serikali, pamoja na mgao unaopatikana kutokana na uvuvi wa bahari kuu, iongeze jitihada ya kutafuta wawekezaji katika eneo la uvuvi wa bahari kuu. Tunaamini kuwa, tukiwa na wawekezaji katika eneo hili tutaweza kuitumia rasilimali yetu ya bahari vizuri na tutaimarisha uchumi wa nchi.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

Kamati inaitaka Serikali kuleta mbele ya Baraza Sheria ya Kuanzishwa Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu ambayo ilipitishwa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kukidhi masharti ya kifungu cha 132 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

UFUGAJI WA SAMAKI NA MAZO YA BAHARINI

Kamati imeridhishwa na mwamko wa wananchi katika kujishughulisha na shuguli za ufugaji wa samaki, jambo hili limepelekea ajira nyingi kwa vijana. Kamati yetu ilibahatika kutembelea mabwawa mbali ya ufugaji wa samaki katika maeneo ya Unguja na Pemba pamoja na kuonana na wafugaji wa samaki. Wafugaji wa samaki wanakabiliwa na changamoto mbali mbali katika shughuli zao.

CHANGAMOTO

(a) Uhaba wa vifaranga vya samaki.

(b) Kutokuwa na taaluma ya kutosha juu mambo mbali mbali ya ufugaji, ulishaji na uwendeshaji wa samaki.

(c) Kutokuwa na kituo cha tafiti za ufugaji wa mazao ya baharini na uvuvi ili kuweza kutatua changamoto.

(d) Wizi wa mazo ya baharini.

(e) Ugumu wa upatikanaji wa mikopo kwa wafugaji wa mazao ya baharini.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Serikali iharakishe mpango wa kujenga bwawa la samaki katika eneo la maruhubi kwa ajili ya uzalishaji wa vifaranga vya samaki ili wafugaji waondokane na changamoto ya ukosefu wa vifaranga.

2. Wizara iendelee kutoa elimu kwa wafugaji wa samaki ili watumie njia za kisasa na za kitaalamu katika kufanya shughuli zao kwa lengo la kuwa na uzalishaji mkubwa wa samaki.

3. Kutokana na kuimarika kwa shughuli za uvuvi na kuhamasika kwa ufugaji wa mazao ya baharini, Serikali iandae mpango wa kuanzisha kituo cha utafiti wa mazao ya baharini ili kiweze kuwasaidia wavuvi na wafugaji wa mazao ya baharini.

4. Wizara kwa kushirikiana na Taasisi zinazohusika, iangalie namna gani itaweza kuwasaidia wafugaji wa mazao ya baharini kupata mikopo.

MRADI WA UJENZI WA SOKO LA SAMAKI – MALINDI

Miongoni mwa juhudi za Serikali katika kuimarisha sekta ya uvuvi nchini ni kuwa na mradi wa ujenzi wa soko la samaki katika eneo la Malindi. Mradi huu unafadhiliwa na Serikali ya Japani na hatua za awali za ujenzi wa soko tayari zimeshaanza zikiwemo pamoja na kuweka miundombini ya maji pamoja na umeme. Ujenzi wa soko hili ulichelewa kuanza kutokana na michoro ya awali kushindwa kukidhi masharti ya majengo ya Mji Mkongwe, suala la michoro tayari limeshapatiwa ufumbuzi na kukubalika na UNESCO.

Ujenzi huu utagharimu jumla ya Tshs.8,000,000,000/- na utachukuwa muda wa miaka miwili hadi kukamilika kweke kwa mujibu wa makubaliano. Utaratibu wa kutafutwa Mkandarasi unaendelea na mara tu atakapo patikana ujenzi utaanza.

Kamati katika ziara yake ya kutembelea eneo hili, lilikutana na wadau wa uvuvi wanaotumia eneo hilo na Kamati ilitaka kujuwa mashirikiano yao na Wizara ya Kilimo. Wadau walieleza kuwa mashirikiano ni mazuri na wako tayari kutoa ushirikiano wowote ili kufanikisha ujenzi wa soko hili. Kamati iliridhika kuona kuwa wananchi wapo tayari kutoa ushirikiano wa dhati kwa Serikali yao ili kukamilisha miradi y maendeleo ya Serikali kwa maslahi ya wananchi.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kabla ya kuanza kwa ujenzi, Wizara ijiridhishe kuwa eneo la ujenzi halitakuwa na athari yoyote ya bahari kwa baadae katika eneo la ujenzi.

2. Tukizingatia kuwa Zanzibar inaelekea katika uchumi wa bahari kuu, soko pia liendane na ujenzi wa kisasa ili kuimarisha uvuvi nchini na kuvutia wawekezaji.

3. Wizara ihakikishe kuwa mradi unasimamiwa vizuri na unamaliza kwa wakati kama itakavyokubaliwa katika mikataba.

4. Wizara itoe mashirikiano mazuri kwa wavuvi wanaotumia eneo hilo wakati utakapoanza ujenzi huo kwa kuwatafutia eneo jengine kwa kipindi chote cha ujenzi wa soko.

SOKO LA SAMAKI LA TUMBE

Kamati imefurahishwa na jitihada za Serikali za kuwajengea wavuvi soko la samaki katika eneo la Tumbe – Pemba, pamoja na kukamilika kwa ujenzi huu Kamati imeona kuwa bado zipo kasoro zinazoonekana katika ujenzi wa soko hili jambo ambalo linaweza kuleta usumbufu kwa watumiaji wa soko hili.

Vile vile, Kamati ilielezwa juu ya mgogoro uliopo baina ya Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni na wavuvi wa eneo hili katika suala zima la mapato yatakayotozwa katika soko hilo, jambo ambalo limepelekea tokea kufunguliwa kwa soko hili limeshindwa kutumiwa hadi hii leo. Kamati inaiomba sana Wizara kuendelea kutumia busara zake ili wananchi waweze kulitumia soko hilo kwani fedha nyingi za wananchi zimeshatumika kwa ajili ya ujenzi wa soko hilo.

Vile vile, Kamati imesikitishwa baada ya kuelezwa kuwa hadi leo mashine ya barafu iliyoletwa kwa ajili ya kutumika katika soko hilo imeshindwa kuingizwa katika chumba chake kutokana na ukubwa wa mashine kushindwa kuingia katika mlango wa chumba hicho.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Busara zitumike ili kuhakikisha wananchi wanalitumia soko la Tumbe.

2. Serikali iangalie uwezekano wa kufanya matengenezo ya kasoro zilizopo ili soko liwe na mazingira mazuri kwa watumiaji wake.

3. Wizara ihakikishe inatafuta njia ya kuingiza mashine ya barafu katika chumba kilichotengwa.

SEKTA YA MIFUGO

Sekta hii inasimamiwa chini ya **Programu ya Maendeleo ya Mifugo,** ambapo jumla ya Tshs. 1,760,746,000/- zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Programu hii**.** Sekta ya mifugo ni miongoni mwa sekta muhimu sana katika nchi, kwani imetoa ajira nyingi kwa wafugaji na kuongeza kipato cha mfugaji. Serikali imekuwa ikichukuwa jitihada mbali mbali katika kuhakikisha sekta hii inaimarika nchini ikiwemo pamoja nan kuanzisha program mbali mbali za kuwapatia wafugaji mifugo ikiwemo ng'ombe, mbuzi na kuku kwa lengo kumuinua mfugaji na kutoa ajira kwa wafugaji. Takwimu zinaonesha kuwa, kuna ongezeko kubwa la uzalishaji wa maziwa na mayai katika kipindi hiki, hii ni kutokana na mwamko wa wananchi wengi kuijiunga katika shughuli za ufugaji.

Katika kutekeleza program hii, vikundi 8 tayari vimepatiwa ng'ombe 160 wa kisasa na mbuzi 360 (Cow shed na Got shed), na vile vile kufundisha mabwana mifugo binafsi wa vijijini 47 kwa upande wa Unguja.

Kamati wakati ikiwa katika kazi zake, ilikutana na wenyeviti kamati za ufugaji kwa upande wa Unguja na Pemba. Katika vikao hivyo wafugaji walieleza changamoto zifuatazo:

CHANGAMOTO

(a) Bei kubwa ya pembejeo za mifugo kama vile vyakula na madawa ya mifugo ambayo inapunguza kasi ya uzalishaji na ukuaji wa sekta ya mifugo.

(b) Kuwepo kwa maradhi ya mifugo.

(c) Tatizo la mabadiliko ya tabia nchi ambalo linasabaisha ukame wa muda mrefu jambo ambalo limepelekea ukosefu wa malisho ya mifugo.

(d) Tatizo la soko la bidhaa za mifugo kama vile mayai na maziwa jambo ambalo linapunguza uwezo na ari kwa wafugaji.
(e) Uhaba wa taaluma kwa wafugaji.

(f) Changamoto ya kutowepo kwa maeneo ya ufugaji.

(g) Uhaba wa madaktari wa mifugo na vitendea kazi.

(h) Uhaba wa vifaa vya maabara ya mifugo.

(i) Tatizo la kupatikana kwa mbegu nzuri za ng'ombe wa maziwa.

(j) Kuwepo kwa maradhi ya kuku jambo ambalo linapelekea kupunguza ari ya ufugajiwa kuku kwa wafugaji.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Serikali iandae utaratibu maalumu wa kudhibiti uingizaji wa bidhaa za mifugo kutoka nje ya nchi hususan zile ambazo zinazalishwa kwa wingi ndani ya nchi.

2. Kuongeza kasi ya utoaji wa elimu kwa wafugaji.

3. Serikali kuongeza ajira kwa wataalamu wa mifugo ili tuwe na wataalamu wa kutosha.

4. Wizara iendelee kutafuta wawekezaji kwa ajili ya kuanzisha viwanda vya kuzalisha pembejeo za mifugo na kilimo ili kupunguza gharama kwa wafugaji.

5. Serikali ianzishe mpango maalumu wa kuhamasisha wananchi kula bidhaa za mifugo kama vile mayai na maziwa ikiwemo pamoja na kuwa na siku maalumu ya kunywa maziwa.

6. Serikali iandae mpango wa kuanzisha kituo cha utafiti wa mifugo ili kufanya tafiti za aina mbali mbali za mifugo.

7. Kutokana na ongezeko kubwa la ukuaji wa sekta ya kilimo sambamba na ukuaji wa sekta ya mifugo, tayari yameanza malalamiko ya maeneo ya ardhi kwa wakulima na wafugaji. Ili kunusuru migogoro ambayo inayoweza kujitokeza hapo baadae, Serikali ianzishe mpango maalumu wa kutenga maeneo ya mifugo.

SHAMBA LA MIFUGO – PANGENI

Katika kuhakikisha sekta ya mifugo inaimarika nchini, Serikali ilitenga eneo maalumu kwa ajili ya shughuli za mifugo ambalo lipo chini ya Wizara ya Kilimo. Shamba linakabiliwa na changamoto ya uvamizi na hadi sasa bado halijapatiwa hatimiliki pamoja na kukamilika kwa taratibu zote za upimaji wa shamba hilo. Shamba hili linasimamiwa na wafanyakazi wa Wizara ya Kilimo na ipo mifugo ya ng'ombe na mbuzi ikiwemo ya Wizara na watu binafsi ambayo inashughulikiwa na wafanyakazi hao. Wakati kamati inatembelea katika eneo hilo, Kamati haikuridhishwa na utaratibu wa ufugaji unaoendeshwa katika eneo hilo.

CHANGAMOTO

(a) Uhaba wa mifugo kulinganisha na ukubwa wa eneo.

(b) Uchakavu wa majengo kwa ajili ya matumizi ya wafanyakazi.

(c) Kukatika kwa uzio wa senyenge jambo ambalo linaweza kupelekea ongezeko la uvamizi katika eneo la shamba.

(d) Ukosefu wa upatikanaji wa maji kwa ajili ya matumzi ya wanaolishughulikia shamba hilo na wanyama.

(e) Uhaba wa malisho ya wanyama.

(f) Tatizo la uvamizi wa shamba kwani baadhi ya watu hupanda miti ya kudumu.

(g) Njia ya kupita kuelekea kwenye shamba ni mbovu sana.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Wizara itafute namna bora zaidi ya kuliimarisha na kuliendeleza shamba kwa lengo la kuimarisha sekta ya mifugo.

2. Wizara iandae mpango maalumu wa kuongeza idadi ya mifugo katika eneo la shamba, mabli ya ushauri wa Kamati kuitaka Wizara kuzuia kuuza mifugo inayozaliwa katika shamba hilo kwa muda. Kwasababu Wizara hii ndio kimbilio la wafugaji wetu, kwahivyo hatuna budi kuwa wanyama wa kutosha.

3. Tatizo la maji katika eneo la shamba limekuwa ni kilio cha muda mrefu, Wizara itafute suluhisho ili maji yaweze kupatikana katika eneo hilo. Kwani kupatikana kwa majiya uhakika kutapelekea pia kuwepo na malisho ya uhakika kwa wanyama.

4. Serikali iharakishe kutolewa kwa hatimiliki ya shamba hilo ili kudhibiti vitendo vya uvamizi katika maeneo ya shamba.
5. Serikali ianzishe mpango maalumu wa kuifanyia matengenezo njia ya kuelekea shamba la Pangeni kwani iko hali mbaya sana na ni usumbufu kwa wanaokwenda katika shamba hilo.

RASILIMALI ZA MISITU NA MALIASILI ZISIZOREJESHEKA

Wizara imeanzisha **Programu inayojulikana Programu ya Maendeleo ya Rasilimali za Misitu na Maliasili Zisizorejesheka** kwa ajili ya usimamizi wa misitu na rasilimali zisizorejesheka, ambapo jumla ya Tshs. 1,667,436,000/- zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Programu hii. Wizara imekuwa ikitekeleza Programu hii kwa ukaribu kwa kushirikiana na jamii pamoja na wanavijiji wanayozunguka maeneo hayo. Kamati ilibahatika kutembelea eneo linalochimbwa mchanga Zingwezingwe kwa upande wa Unguja na Shumba kwa upande wa Pemba na vile vile eneo linalochimbwa mawe Vitongoji – Pemba ili kuona ni kwa kiasi gani Wizara inasimamia rasilimali hizi.

Wizara imechukuwa juhudi mbali mbali kwa kushirikiana wananchi katika kukomesha matumizi ya msumeno wa moto ambao ndio adui mkubwa wa misitu na miti yetu tulionayo. Vile vile, katika kuhakikisha rasilimali zisizorejesheka zinatumika vizuri kwa ajili ya matumizi kwa vizazi vijavyo, Wizara tayari imeshaweka mpango maalumu wa matumizi ya rasilimali ya mchanga ili kuzuia uchimbaji mchanga kiholela. Tafiti zinaonesha kuwa katika kipindi cha 2005 hadi 2015 jumla ya hekta 522 zimeshachimbwa mchanga kwa upande wa Unguja na hekta 150 kwa upande wa Pemba. Tukizingatia kuwa nchi yetu ni kisiwa na tunahitaji ardhi kwa matumizi mbali mbali ikiwemo kwa shughuli za makaazi, kilimo, ufugaji na shughuli nyengine mbali mbali kuna haja ya kuwa na matumizi bora ya ardhi zetu sambamba na nidhamu za matumizi ya maliasili zisizorejesheka. Naomba nikumbushie msemo maarufu unaosema kuwa ***"Hatukurithi ardhi hii kutoka kwa mababu zetu bali tumeazimwa na wajukuu zetu".*** Katika kusimamia Rasilimali za Misitu na Maliasili Zisizorejesheka zipo changamoto zifuatazo:

CHANGAMOTO

(a) Tatizo la matumzi ya msumeno wa mto bado linaendelea.

(b) Uchimbaji wa maliasili kiholela.

(c) Uharibifu wa mazingira.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Wizara kwa kushirikiana na Taasisi husika iendelee kukomesha matumizi ya msumeno wa moto.
2. Kuwe na usimamizi mzuri juu ya taratibu za uchimbaji wa maliasili zisizorejesheka.
3. Serikali ianzishe sera maalum ya Green Policy ili tuweze kupanda miti kwa wingi katika nchi kwa ajili ya kuhifadhi mazingira yetu. Mfano wa nchi iliyofanikiwa kupanda mingi ni Korea na China ambao wanatumia sera hiyo.
4. Wizara itoe elimu kwa wanajamii na hata kwa wanafunzi juu ya umuhimu wa upandaji miti na athari za ukataji wa miti.
5. Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, itoe taarifa maalumu mbele ya Baraza hili kuhusu "Hali halisi ya uchimbaji mchanga Zanzibar" ili Wajumbe wa Baraza hili pamoja wananchi waelewe dhamira ya Serikali juu ya matumizi ya rasilimali ya mchanga.

MSITU WA JOZANI

Msitu wa Jozani ndio msitu mkubwa kwa Zanzibar ukifuatiwa na msitu wa ngezi ulioko Pemba. Wanaotembelea katika msitu huu wamekuwa wakiongezeka siku hadi siku, ingawaje idadi ya wananchi wanaotembelea bado ni ndogo ikilinganishwa na wanaotoka nje ya nchi, hii inatokana na wananchi kutokufahamu thamani ya rasilimali ya misitu tuliyonayo.
Kamati iliiagiza Wizara kufanya mapitio ya tozo kwa wanaoingia katika msitu, Kamati imeridhishwa na utekelezaji wa agizo hili kwani tayari imeshaandaa orodha ya mpya ya malipo kwa watakaotembelea katika msitu.

Kuanzia Januari 2016 hadi Disemba jumla ya shilingi **852,872,781** zimepatikana kama ni mapato yatokanayo na msitu. Mapato hayo yanatokana na wageni waliotembea katika msitu wapatao **52,799** ambao kati ya hao **9,085** kutoka ndani ya nchi na **43,714** kutoka nje ya nchi. Hii ni kuonesha kuwa endapo kutakuwa na miundombinu mizuri na kuzidi kuutangaza msitu ndani na nje ya nchi mapato yataongezeka zaidi. Mgao wa mapato katika msitu unakwenda katika maeneo yafuatayo:

(a) Jumuiya ya Wenye Mashamba-Jozani
(b) Jumuiya ya Hifadhi MazingiraJozani
(c) Miradi ya maendeleo vijijini.
(d) Kamati ya uhifadhi kijiji cha Pete
(e) Idara ya Misitu
(f) Hifadhi ya Taifa Jozani-Chwaka

Katika kipindi cha Julai hadi Disemba, 2016 Msitu umeshaingiza jumla ya Tshs. **483,759,700.00** kati ya hizo Tshs. **88,975,871.00** zimeingizwa katika Idara ya Misitu ambazo ni sawa na asilimia 18.39 ya makusanyo.

Msitu unakabiliwa na changamoto zifuatazo:

CHANGAMOTO

1. Uhaba wa mbinu mbadala wa kipato kwa Wanajamii:
   Wanajmii wanakabiliwa na uhaba wa mbinu tofuati mbadala wa kutotegemea msitu (kwa kuni, miti ya kujengea na mkaa), licha ya kupatiwa mgao wa fedha za utalii Jozani kwa maendeleo ya jiamii husika. Miongoni mwa mbinu zilizoibuliwa na IMMZ kupitia Uongozi wa Hifadhi Taifa, Jozani-Ghuba ya Chwaka ni Kilimo cha kisasa cha mazao ya chakula katika maeneo ya ardhi ya maweni ikiwemo mboga mboga, ufugaji nyuki, n.k.

2. Usafifiri wa gari usiokuwa na uhakika:
   Gari iliyopo ni mbovu na haimudu mikiki ya kazi za ulinzi (Patroo) na mashambani.

3. Mawasiliano ya Mtandao (Internet);
   Watalii na hata kwa matumizi ya Ofisi huduma hii inahitajika lakini mazingira ya Kijografia ya Jozani inawiya vigumu kuweka mitambo kwa kutumia mitandao iliyopo Zanzibar *(Zantel, Mobitel, Vodacom, Helotel, n.k).*

4. Uhaba wa wafanyakazi:
   Hivi sasa wapo wafanyakazi walinzi 13, ilhali wanaohitajika si chini ya 25. Na mahitaji halisi ya wafanyakazi waajiriwa wa kuongoza watalii ni 12, ilhali waliopo ni waajiriwa sita (6) tu.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Wizara iendelee kutoa elimu ya kutosha katika maeneo mbali mbali ili kuhamasisha wananchi kutembelea katika msitu sambamba na kuutangaza msitu ndani na nje ya nchi.

2. Pamoja na kuanzisha utaratibu mpya wa malipo, Kamati inaitaka Wizara kukaa na kuangalia upya mgao wa mapato unaoingia katika Idara ya misitu kuwa jee Idara inastahiki kupata mgao huo.

3. Kwakuwa Msitu unao mgao wake kwa ajili ya kuendesha shughuli za Msitu, Kamati inaagiza itumie fedha hizo kutatua changamoto zake kwa kuunaganisha internet.

4. Wizara iandae mpango wa kupatikana usafiri wa uhakika kwa ajili yam situ.

5. Wizara iandae mpango wa kuongeza nafasi za ajira za wafanyakazi wa msitu.

MSITU WA NGEZI

Kamati ilitembelea msitu wa Ngezi Pemba na kupokea taarifa kuhusu maendele ya msitu. Kwa ujumla maendeleo ya msitu yanaridhisha kutokana na kuongezeka kwa idadi ya wanaotembelea msitu siku hadi siku. Lakini tukilinganisha na idadi ya wanaotembelea msitu wa Jozani bado kuna upungufu mkubwa sana kwa watu wanaotembelea msitu huo wa ndani na nje ya nchi.

Msitu huu unakabiliwa na Changamoto zifuatazo:

CHANGAMOTO

(a) Njia ya kuelekea kwenye msitu ni mbovu.

(b) Uchakavu wa majengo yanayotumiwa na wafanyakazi.

(c) Uhaba wa wafanyakazi wakiwemo walinzi ikilinganishwa na ukubwa wamsitu.

(d) Mwamko wa wananchi kutembelea katika msitu bado ni modogo.

(e) Matokeo ya ukataji miti kwa baadhi ya maeneo.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Serikali kwa kushirikiana na Halmshauri ya Wilaya ya Micheweni iangalie uwezekano wa kuijenga njia ya kuelekea msitu wa Ngezi.

2. Wizara kupitia mapato yanayotokana na msitu ijenge majengo kwa ajili ya wafanyakazi ili mandhari ya eneo iweze kuwavutia wanaotembelea.

3. Wizara iongeze jitihada za kuutangaza msitu ndani na nje ya nchi.

4. Uongozi wa msitu uendelee kutoa mahirikiano ya karibu na wanavijiji wanaouzunguka msitu ili wawe ni walinzi wa msitu.

MSITU WA MASINGINI

Kamati ilitembelea eneo la msitu wa Masingini ambalp ndani yake imeanzishwa “City Park”. Kamati imeridhishwa na juhudi za Wizara kwa kubuni uanzishwaji wa city park katika msitu wa masingini kwa lengo la kuwavutia wananchi na watalii wanaotembelea Zanzibar.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Wizara iongeze juhudi ya kupanda miti ya asili katika eneo la msitu.

2. Wizara iangalie uwezekano wa kuanzisha mkahawa (restaurant) ambayo itakuwa na vyakula vya asili tu kama vile muhogo, viazi, mashelisheli, n.k ili uweze kujitangaza zaidi.

3. Wizara iendelee kutumia wataalamu wake ili kubuni vivutio vyengine kwa watalii na wananchi wanaokwenda kutembelea kwenye msitu.

MIPANGO NA UTAWALA WA KAZI ZA WIZARA

Wizara imeandaa **Programu maalumu ya Mipango na Utawala wa Kazi za Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi** kwa ajili kusimamia shughuli zote za utawala chini ya Wizara, ambapo jumla ya Tshs. 19,481,647/- zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Programu hii.. Katika kutekelezaji wa Programu hii, Wizara imesimamia shughuli mbali za kiutawala chini ya Wizara hii.

Niukweli usiopingika kuwa Wizara ya Kilimo ni moja Wizara ambayo inao wataalamu wengi sana katika sekta ambazo zinasimiwa na Wizara hii kulinganisha na Wizara na nyengine. Hata hivyo, upungufu wa wataalamu umekuwa ni changamoto kubwa kutokana na kukuwa kwa sekta zinazosimamiwa na Wizara. Vile vile, kuna changamoto ya wataalamua ambao wanasomeshwa na Wizara kuchukuwa likizo bila ya malipo au kuondoka kazini na hivyo kushindwa kutumia utaalamu wao katika Wizara.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Wizara inayohusika na utumishi wa umma, itoe vipaombele vya ajira kwa wataalamu wa kilimo, mifugo na uvuvi ili kuimarisha sekta hizo nchini.

2. Wizara ihakikishe watumishi wote waliondoka na vyombo vya moto vya Wizara vinarudishwa Wizarani.

3. Wizara itafute njia bora ya kuhakikisha kuwa takwimu zinazotolewa na Wizara zinakuwa sahihi, na tuondokane na utaratibu wa kimazoea wa kufanya takwimu.

4. Wizara iandae utaratibu maalumu ili kuhakikisha kuwa wataalamu wanaosomeshwa na Wizara wanazitumia taaluma kwa ajili ya kuimarisha shughuli za Wizara.

SHAMBA LA MAKURUNGE - BAGAMOYO

Kamati katika vikao mbali mbali na Wizara, imekuwa ikilizungumzia mara kwa mara shamba hili kutokana na khofu ya kupotea kama ambavyo hekta nyingi sana zilizokuwa zinamilikiwa na Serikali zimepotea. Kamati imeelezwa kuwa tayari Serikali zote zimeshakubaliana juu ya umiliki na matumizi ya shamba hilo, hata hivyo ukutokana na gharama za upatikanaji wa hatimiliki bado Wizara inaendelea kujipanga. Kinachofanyika sasa hivi ni kutafuta mshauri elekezi kwa ajili ya kuishauri Wizara namna bora ya matumzi ya shamba hili kwa mujibu wa mipango miji wa eneo hilo.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Mara baada ya mshauri elekezi kuwasilisha maoni yake na kuangaliwa kwa kina na Wizara, Wizara aindae mpango wa haraka wa matumizi ya shamba hilo.

2. Wizara ikae na Taasisi za Fedha za SMZ ikiwemo ZSSF na Shirika la Bima kuona namna gani wanaweza kuliendeleza shamba hilo kwa ajili ya kuwekeza.

3. Wizara iwe na mpango wa baadae wa kutafuta hatimiliki ya shamba hilo.

OFISI KUU PEMBA

Katika bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017 Afisi kuu Pemba imepangiwa kukusanya jumla ya Tshs. 570,420,000/- . Katika kipindi cha Julai hadi Septemba, 2016, Afisi imekusanya jumla ya Tshs. 27,276,400/- sawa na asilimia 4.78 ya lengo. Na kipindi cha Oktoba hadi Disemba, 2016/2017 Afisi imekusanya jumla ya Tshs. 56,962,450/- sawa na asilimia 9.99 ya lengo.

Kwa ujumla, hali ya ukusanyaji wa mapato kwa upande wa Pemba sio nzuri ikilinganishwa na mapato yaliyokusanywa na malengo ya makusanyo kwa mwaka. Kamati inaitaka Afisi kuongeza jitihada za ukusanyaji wa mapato kwani tunaamini uwezo wa kufikia au kupindukia malengo ya makusanyo yaliyokusidiwa yanaweza kufikiwa endapo kutakuwa mikakati imara ya kuhakikisha mapato ya Wizara yanakusanywa ipasavyo.

Kwa upande wa Matumizi, Afisi Kuu Pemba katika kipindi cha Julai hadi Septemba, 2016 Afisi iliomba kuingiziwa Tshs. 679,014,650/- kwa ajili ya mishara na kilichopatikana ni 679,014,650/- ambazo ni sawa asilima 100. Vile vile, kwa upande wa matumizi ya kawaida (OC) Afisi iliombwa kuingiziwa jumlam ya Tshs. 113,811,000/- na kilichopatikana ni 113,811,000/- ambazo ni sawa asilimia 100.

Katika kipindi Oktoba hadi Disemba,2016 Afisi aliomba kuingiziwa jumla ya Tshs. 679,014,650/- kwa ajili ya mishara na kilichopatikana ni 679,014,650/- ambazo ni sawa asilima 100. Vile vile, kwa upande wa matumizi ya kawaida (OC) Afisi iliombwa kuingiziwa jumlam ya Tshs. 138,651,508/- na kilichopatikana ni 114,000,000/- ambazo ni sawa asilimia 83.7.

Kwa upande wa fedha za maendeleo, jumla ya Tshs. 86,110,000/- ziliingizwa katika robo ya kwanza na Tshs. 41,000,000/- ziliingizwa katika robo ya pili.

Kwa ujumla, kwa upande Wizara ya Kilimo, Afisi Kuu Pemba uingizwaji wa fedha ni mzuri tunaiomba sana Serikali uingizwaji huu wa fedha uendelee kwa lengo la kuimarisha sekta za kilimo, mifugo na uvuvi kwa upande wa Pemba.

CHANGAMOTO

(a) Kuwepo kwa idadi ndogo ya wafanyakazi katika madiko, vitalu pamoja na vituo vya huduma za mifugo wakiwemo wataalamu hali inayopelekea utoaji wa huduma hafifu, kukosekana ukusanyaji wa mapato na uzalishaji mdogo.

(b) Ushirikishwaji mdogo kwa baadhi ya maafisa wakuu katika Idara zao wakati wa kupanga bajeti, jambo linapelekea kuzorotesha utekelezaji wa kazi za msingi za Idara husika kwa upande wa Pemba.

(c) Kuwepo kwa deni la stahiki la wafanyakazi kiasi cha Tshs. 128,000,000/- kwa waliokwenda lilizo.

(d) Ukosefu wa Mwanasheria kwa Afisi Kuu Pemba.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Wakati Wizara itakapotoa nafasi za ajira kwa Wizara ya Kilimo iangalie pia upungufu wa wafanyakazi uliopo kwa upande wa Pemba.

2. Wizara ihakikishe inatoa ushirikiano katika kipindi chote cha uandaaji wa bajeti kwa wakuu wa Idara wa Afisi Kuu Pemba.

3. Afisi iendelee kutumia OC zake kwa ajili ya kupunguza madeni ya wafanyakazi.

4. Wizara ihakikishe anapatikana Mwanasheria katika Afisi Kuu Pemba kwani zipo changamoto nyingi za kisheria ambazo zinahitaji uwepo wa mwanasheria.

TAASISI YA UTAFIITI WA KILIMO – PEMBA

Taaisisi hii ipo Chini ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ya Zanzibar iliyopo chini ya Wizara ya Kilimo. Taasisi hii ni muhimu sana kwa maendeleo ya kilimo nchini. Kamati ilifika katika eneo la kituo lililopo Matangatuani – Pemba na kujionea maendeleo ya kituo hicho. Hata hivyo, kituo kinakabiliwa na changamoto zifuatazo.

CHANGAMOTO

1. Upungufu wa wataalamu katika kituo cha utafiti na wafanyakazi.

2. Uhaba wa fedha za kufanyia tafiti.

3. Tatizo la mabadiliko ya tabia nchi ambalo linaathiri shughuli za kituo. Hata hivyo, kituo kimeanza na mfumo wa umwagiliaji maji kwa njia ya matone (drop irrigation).

4. Kutokuwepo kwa ukuta katika eneo la kituo, jambo ambalo linahatarisha usalama wa kituo.

5. Ukosefu wa vifaa vya maabara.

6. Ukosefu wa mawasiliano kwa njia ya mtandao.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Wizara iendelee kusomesha wataalamu wake kwa ajili ya kuwajenga ili waweze kufanya tafiti za kilimo.

2. Serikali iongeze bajeti ya taasisi hii ili iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi.

3. Wizara iangalie uwezekano wa kujenga ukuta katika eneo la kituo ili kuliweka katika hali ya usalama.

4. Serikali itafute vifaa vya maabara kwa ajili ya uwendeshaji wa shughuli za kituo.

5. Wizara itenge fedha kwa ajili ya kuunganisha huduma za mtandao katika eneo la kituo.

SEHEMU YA TANO

HITIMISHO

Kwa ujumla Kamati imefanikisha majukumu yake ya kufuatilia utekelezaji wa kazi zake ilizojipangia katika Wizara na taasisi zilizo chini ya Wizara hizo zilizoainishwa katika ripoti hii. Kamati inazipongeza Wizara na taasisi hizo kwa mashirikiano yao ya dhati kwa Kamati katika kufanikisha kazi zake pamoja na juhudi zinazochukuliwa katika utekelezaji wa kazi zao.

Kamati pia inapenda kutoa shukurani kwa wale wote waliofanikisha kazi za Kamati kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na pia kuwezesha taarifa za Kamati kutayarishwa na kuwasilisha kunakohusika. Kamati inawashukuru kwa dhati viongozi na watendaji wote wa Serikali na wa Baraza pamoja na wale wote waliofanikisha kazi za Kamati.

XXXXXXXXX *mwisho* XXXXXXXXXXX